SUPA JACKPOT
TZS. 1,067,615,605
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



BINTI adaiwa kujinyonga kisa karipio la wazazi wake

UKURASA 2




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Januari 21, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581197

www.ippmedia.com

...ANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
...uardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


## Ndugai aibuka na hoja mpya

UKURASA 2



Spika mstaafu Job Ndugai

UKURASA WA 3

### WATU KUMI MBARONI MADAI UCHAKACHUAJI WA MBOLEA

JESHI la Polisi mkoani Njombe linawashikilia zaidi ya watu 10, wakiwamo wanafamilia kwa tuhuma za kuchakata mbolea feki kisha kuwauzia wakulima katika mtaa wa Mgodechi, Halmashauri ya Mji wa Njombe. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi (ACP) Hamisi...

UKURASA WA 3

### CCM YAIBUA SAKATA VISHIKWAMBI KWA WALIMU

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimetoa wiki moja kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuanzia jana kuhakikisha vishikwambi vilivyotolewa na serikali kwa ajili ya walimu, vinawafikia walengwa.
CCM imesema imepokea malalamiko ya kutotekelezwa kikamilifu kwa...



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akizungumza na mwigizaji maarufu wa filamu duniani kutoka Uingereza, Idris Elba (wa pili kulia), ambaye ni balozi wa hisani wa Umoja wa Mataifa wa IFAD na mke wake, Sabrina Elba (kulia), walipokutana Davos, Uswisi wiki hii. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 18

### ACT YASHTUKIA JAMBO MFUMO WA RUZUKU KATIKA MBOLEA NCHINI

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kutengeneza mazingira rafiki ili kuvutia wawekezaji zaidi kwenye uzalishaji wa mbolea nchini na kuviimarisha viwanda vilivyoko.
Pia kimeitaka serikali kubadili mfumo wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa kuiondoa kwa wasambazaji na badala yake iweke ruzuku hiyo kwenye...

## 50,000 wajitosa nafasi 500 za ajira za Polisi

UKURASA 10

## Wachukua hatua kuinusuru shule yenye mazingira hatarishi kiafya

UKURASA 4

**MICHEZO** WACHEZAJI YANGA KATIKA DOZI MPYA UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Imamu Mkuu wa Msikiti wa Masjid Mnyamani Buguruni, Sheikh Mohamed Iddi Mohamed, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitahadharisha kuhusu mjadala wa kimadhehebu kati ya waislamu wa Ki-Shia na Ki-Sunni, usipelekee katika tishio la uvunjifu wa amani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ndugai aibuka na hoja mpya kwa Watanzania

**Paul Mabeja na Peter Mkwavila,** DODOMA

SPIKA mstaafu Job Ndugai amewataka Watanzania kutoitegemea serikali kwa kila kitu, bali kila mmoja atimize wajibu wake katika kushiriki shughuli mbalimbali za kujipatia kipato ili kujikwamua kiuchumi.

Ndugai alitoa kauli hiyo jana jijini hapo alipozungumza kwenye mkutano wa kutangaza mafanikio ya serikali ya awamu sita kwa kipindi cha miaka miwili ya kuwa madarakani.

"Katika maisha yetu ya kawaida, yapo mambo hufanywa na serikali kwa sababu hayawezi kufanywa na mtu mmojammoja, ndiyo mfumo wa utawala wa nchi.

"Haiwezekani kila mtu awe na shule kwa ajili ya watoto wake na analipa walimu mwenyewe kwa sababu hilo haliwezekani, ndiyo maana linakuwa ni jukumu la serikali.

"Haiwezekani kila mmoja wetu akajenga reli yake, jamani inawezekana? Ndio maana serikali inafanya, ndiyo kazi ya serikali. Pia haiwezekani kila mmoja wetu awe na stoo yake ya dawa, yote hufanywa na serikali kwa maana serikali ndiyo mama, ndiyo baba. Unaweza kuwa na panadol lakini zile nyingine siyo rahisi," Ndugai alifafanua.

Mbunge huyo wa Kongwa mkoani Dodoma alisema wananchi wanao wajibu wa kuhoji mambo yanayopaswa kufanywa na serikali na wana kila sababu ya kufanya hivyo kwa mujibu wa Katiba, lakini wao pia wanapaswa kuhakikisha yale yanayowahusu wanayatekeleza kikamilifu.

Ndugai aliongeza kuwa haiwezekani serikali ikajenga shule kisha yenyewe ikawa na jukumu la kumpeleka mtoto shuleni na kumrudisha nyumbani.

"Serikali inajenga hospitali lakini wewe mgonjwa wako unamficha ndani, serikali haiwezi kupita kila nyumba kuuliza 'kuna mgonjwa hapa?' Ni wewe ndiye mwenye jukumu la kumpeleka hospitalini mgonjwa wako kwa ajili ya matibabu," alifafanua zaidi Ndugai.

Vilevile, alisema wananchi wanapaswa kufanya shughuli za kiuchumi kwa kuwa ni jukumu lao, vinginevyo wataendelea kubaki nyuma kwa umaskini.

"Twendeni tukafanye shughuli za kiuchumi, ni jukumu letu tukafuge kwa kadri tunavyoweza, serikali itatusadia majosho kwa sababu siyo kila mtu anaweza kuwa na josho lake, itatusaidia baadhi ya dawa na huduma za ugani, tukalime mashamba yetu, serikali itatusaidia dawa za kilimo na mbegu bora inapowezekana," alihimiza.

**KATIBA YA NCHI**

Kimsingi, alichokisema Ndugai jana kimeelekezwa kwenye Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Toleo la Mwaka 1977.

Ibara ya 8(1) ya Katiba inaelekeza: "(a) wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote, na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii".

"(b)lengo kuu la serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi; (c) serikali itawajibika kwa wananchi; (d) wananchi watashiriki katika shughuli za serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii".

**ULIPAJI KODI**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, akifungua mkutano huo kwa niaba ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliwataka Watanzania kuendelea kulipa kodi na tozo kwa maendeleo ya taifa.

"Nichukue fursa hii kumpongeza Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kipindi hiki cha miaka miwili tangu aingie madarakani, uchumi wetu umeendelea kuimarika siku hadi siku," alisema.

Aliwataka vijana kuchangamkia fursa zilizoko katika sekta ya kilimo kwa kuhakikisha kila eneo la ardhi ambalo linafaa kwa kilimo, linalimwa ili kuongeza uzalishaji na kuwa na uhakika wa chakula.

Angellah pia aliwataka machinga kuhakikisha wanahamia bila usumbufu kwenye maeneo ambayo serikali imewekeza fedha nyingi kuwajengea.

# Binti adaiwa kujinyonga kisa karipio la wazazi

**Na Francis Godwin,** IRINGA

ALIYEKUWA mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kihesa, Manispaa ya Iringa, Winifrida Mdindile (17), amefariki dunia akidaiwa kujinyonga baada ya kupewa karipio na wazazi wake na kukosa mahitaji ya mtoto wake.

Winfrida, mkazi wa Semtema A, alikatisha masomo yake baada ya kupata ujauzito.

Rafiki wa karibu na Winifrida, Prince Salila ambaye pia ni mkazi wa Semtema A, alidai: "Winifrida ni rafiki yangu na jana (juzi) nilikuwa naye dukani kwangu mpaka saa mbili usiku, tuliongea mambo mengi na kushauriana ila sikufikiria kama angefikia uamuzi huu wa kujinyonga kwa kuwa nilimshauri sana.

"Asubuhi nilimpigia simu kumjulia hali kutokana na yale aliyonielezea kuwa toka alipopata ujauzito, familia yake ilimtenga na kumwona hana thamani tena."

Baba mzazi wa marehemu, Petro Mdindile, alisema alibaini tukio hilo juzi asubuhi alipoamka na kumkuta mwanawe huyo amejinyonga kwenye mti ulioko nyuma ya nyumba yao na kumwacha mtoto wake mwenye umri wa mwaka na miezi sita akicheza na mtoto mwingine wa familia hiyo.

Mdindile alidai kuwa siku moja kabla ya tukio hilo, binti yake alichelewa kurejea nyumbani na kama mzazi, alimwonya kuhusu tabia na kumtaka aiache ili asimamie malezi ya mtoto wake.

Alisema alifanya hivyo lakini hakufahamu kama binti yake alijisikia vibaya kutokana na karipio hilo alilompatia.

"Jana (juzi) alichelewa sana kurudi nyumbani, alirudi usiku na alikuwa amemwacha mtoto wake hapa (nyumbani) na nilimuuliza 'ulikuwa wapi?' na nilimtaka aache tabia hiyo ili kumlea mtoto wake kwa kuwa ameanza kutembea, hivyo anahitaji uangalizi sana," alisimulia Mdindile. Mwenyekiti wa Semtema A, Rabi Mgata alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kutoa rai kwa wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao kuanzia shuleni hadi nyumbani kwa kufuatilia maendeleo yao pamoja na kujua changamoto zinazowakabili ili kuwaepusha na matukio hatarishi.

"Wazazi wengi wamekuwa 'bize' mpaka wanasahau wajibu wao kwa watoto, jambo ambalo linasababisha watoto wengi kuharibika hivi sasa.

"Ikifika jioni utakutana na mabinti wadogo wanazurura mtaani na nguo za ajabu halafu wazazi hawana habari kabisa.

"Kama unaona mtoto amekushinda ni bora ukatafuta wataalamu waongee naye ili kumnasuru na majanga na siyo kuwa mkali kupita kiasi au kumtenga," alisema.

Nipashe ilishuhudia askari watano wa Jeshi la Polisi (mmoja akiwa na sare rasmi) wakifika eneo la tukio na kuuchukua mwili wa marehemu kwa ajili ya hatua za dola.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi, alipotafutwa na Nipashe ili kuzungumzia tukio hilo, simu yake iliita bila kupokelewa.


**KUPOTEA KWA CERTIFICATE**

**ELIZABERT JONATHAN KASIMILA** Anatangaza kupotelewa na Certificate of organization chenye jina la **TABORA DEVELOPMENT FOUNDATION** kimepotea wiki tatu zilizopita kwa Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa polisi: **DOD/DOD/RB/28478/2023.**

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MOROGORO MUNICIPAL**
**In reference, please quote:**
**Ref,NO. MMC/LD/1981/12......................DATE:16/01/2023**
**YAH:KUUNGULIWA NA BARUA YA TOLEO NA. MMC/LD/198181/9/CG**

**Mada tajwa apo juu yahusika,**

Kiwanja namba 11 kitalu E msamvu morogoro kilitolewa kwa ndugu, **JUSTUS JACKSON MUKURASI wa S.L.P 44, Morogoro** kupitia BARUA YA TOLEO NA. MMC/LD/198181/9/CG kwa muda wa miaka 33 ikiazia tarehe 16/08/2007 mmiliki tajwa hapo juu aliunguliwa na nyumba ake trh 05/12/2022. Kupitia sheria ya ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 Ofisi ya kamishna msaidizi wa Ardhi mkoa wa morogoro inakusudia kuendelea na mchakato wa kummilikisha katika hatua hii hati ndugu JACKSON MUKURASI. Hivyo mtu yeyote mwenye pingamizi au maslahi juu ya kiwanja hiki anatakiwa kutoa taarifa kwa kamishna msaidizi wa Ardhi mkoa wa Morogoro ndani ya siku 30 kuazia tarehe ya tangazo hili.
Valency H.K

Valency H.K
Afisa Ardhi Mteule wa Manispaa ya Morogoro

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MOROGORO MUNICIPAL**
**In reference, please quote:**
**Ref,NO. MMC/LD/23722......................DATE:11/01/2023**
**YAH:NIA YA KUFANYA MAREKEBISHO HATI NAMBA 85071 YA KIWANJA NAMBA 217 KITALU M KIHONDA**

**Mada tajwa apo juu yahusika,**

Kiwanja namba 217 kitalu M Kihonda kilitolewa kwa ndugu AUDIFAX ALOISE CHOMA wa S.L.P 120 Morogoro kupitia hati namba 85071. Miliki hyo ilitolewa kimakosa kwani mmiliki wa kwanza ni ndugu MAJALIWA HAMADI SAID wa S.L.P 120 Morogoro ambaye ana barua ya toleo ya trh 01/04/2009 na ndiye mmiliki halali wa kiwanja tajwa. Ofisi ya mkurugrnzi Manispaa ya Morogoro ina nia ya kufanya marekebisho ya hati iyo kwa kumuondoa AUDIFAX ALOISE CHOMA wa S.L.P 7449 na kummilikisha ndugu MAJALIWA HAMADI SAIDI wa S.L.P 120 Morogoro. Hivyo mtu yeyote mwenye pingamizi au maslahi juu ya kiwanja hiki anatakiwa kutoa taarifa kwa kamishna msaidizi wa Ardhi mkoa wa Morogoro ndani ya siku 30 kuazia tarehe ya tangazo hili.

Valency H.K
Afisa Ardhi Mteule wa Manispaa ya Morogoro

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......01/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: IDRISA MUHUDINI IDDI WA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA MARIAM IDDI MUHUDINI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 23 Mwezi 01 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 10 mwezi 01 mwaka 2023

HAKIMU MFAWIDHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa Wa Morogoro**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 992 YA 2022**
**MZUMBE UNIVERSITY.............................MLETA MAOMBI**
**DHIDI**
**M/S KYUNGU CO.LTD.................................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**HILDA BENEDICT JOHN**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza za Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 23/01/2023 mbele ya mwenyekiti M .KHASIM wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilzwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 19 Mwezi January 2023



Meneja Uhusiano wa Kampuni ya Mabati ya ALAF Limited, Hawa Bayuni, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu hafla ya utoaji wa Tuzo ya Kiswahili ya Safari–Comell ya Fasihi Afrika, zinazotarajiwa kufanyika mwezi huu. Kushoto ni Ofisa Uhusiano wa kampuni hiyo, Theresia Mwasy. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watu 10 mbaroni madai uchakachuaji mbolea

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi mkoani Njombe linawashikilia zaidi ya watu 10, wakiwamo wanafamilia (majina yamehifadhiwa) kwa tuhuma za kuchakata mbolea feki kisha kuwauzia wakulima katika mtaa wa Mgodechi, Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi (ACP) Hamisi Issah, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa watu hao wanadaiwa kuhusika katika kusafirisha vyombo vilivyokuwa vikitumika kuchakachua mbolea, yakiwamo majenereta.

Issah alisema Jeshi la Polisi linaendelea kufanya uchunguzi ili kuwabaini wahusika wengine ili wapelekwe mahakamani na sheria ifuate mkondo wake.

Aidha, aliwashukuru viongozi wote akiwamo mkuu wa mkoa, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) na wananchi kwa kutoa ushirikiano uliosababisha kukamata vitu vinavyohusika na uchakachuaji huo.

"Kuna zaidi ya watu 10 wamekamatwa na hii inahusisha watu wenye vyombo ambavyo vimesafirisha na watu ambao kwa namna moja au nyingine walihusika kubeba jenereta na mambo wengine," alisema Issah.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, aliowataka wafanyabiashara na mawakala wa mbolea mkoa wa Njombe wajue serikali inafuatilia kwa karibu suala la mbolea kwa sababu Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha nyingi kwa ajili ya kubeba dhamana ya ruzuku ya mbolea ya wakulima.

Mtaka alisema sasa inapotokea mfanyabiashara anaingia kwenye tamaa na amepewa leseni na mamlaka za serikali na kufika mahali kukodisha nyumba, majenereta na kununua mashine ili kutengeneza mbolea feki na kupeleka kwa wakulima ni kufedhehesha serikali.

"Wananchi wanatukana serikali kwamba kuna mbolea ya ruzuku kumbe feki. Tunalishukuru na kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kuiheshimisha serikali na tunaomba moyo huu wa askari wetu na vyombo vyetu vyote vya ulinzi na usalama uendelee ili tuweze kuwasaidia wananchi," alisema Mtaka.

Mkurugenzi Mtendaji wa (TFRA), Dk. Stephan Ngailo, alisema mamlaka hiyo imemfutia leseni mfanyabiashara wa mkoani Njombe ambaye anadaiwa kuchakachua mbolea na kuwauzia wakulima kinyume cha utaratibu.

Ngailo alisema pamoja na kumfutia leseni mfanyabiashara huyo, ameomba vyombo vingine kuchukua sheria ili kufikishwa mahali panapostahili.

Alisema mfanyabiashara huyo akikamatwa anatakiwa kuwafidia wakulima wote ambao wameathirika kwa tabia na vitendo vyake hivyo.

Dk. Ngailo alisema lililofanyika mkoani Njombe chini ya usimamizi wa Mkuu wa Mkoa, Mtaka, lifanyike katika mikoa mingine yote nchini hasa Nyanda za Juu Kusini na mkoa wa Kigoma ili kubaini tatizo kama ambalo limejitokeza mkoani hapo.

"Nawashukuru mkuu wa mkoa na timu yako kwa kufanikisha kukamatwa kwa huyu ambaye alikuwa anafanya ubadhirifu, udanganyifu na uhujumu uchumi. Ni wazi kuwa hana nia njema na wakulima, wizara yetu ya kilimo na serikali," alisema Dk. Ngailo.

# CCM yaibua sakata vishikwambi kwa walimu

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimetoa wiki moja kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuanzia jana kuhakikisha vishikwambi vilivyotolewa na serikali kwa ajili ya walimu, vinawafikia walengwa.

CCM imesema imepokea malalamiko ya kutotekelezwa kikamilifu kwa maelekezo ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuhusu ugawaji wa vishikwambi hivyo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema, alisema wakati akizindua ugawaji wa vishikwambi hivyo, Novemba, mwaka jana, Waziri Mkuu Majaliwa aliagiza vifaa hivyo viipelekwe kwa walengwa.

"Ulitengwa muda maalumu wa kutolewa kwa vishikwambi hivi ambao ulikuwa unaishia Januari 15, mwaka huu. Lakini chama kimepokea malalamiko kwamba hadi leo (jana) kuna baadhi ya makundi hayajapata hivyo vishikwambi.

"Lakini kuna baadhi ya wilaya hawajagawa kabisa vishikwambi hivyo. Kuna maeneo mengine unakuta walimu wako 10 na wote wanahitaji na wanastahili kupata, lakini unakuta vishikwambi vinatoka vinane wawili wanaachwa," alisema.

"Chama kinatoa maelekezo, kinaielekeza wizara husika kuhakikisha jambo hili linakamilika na walengwa wote wanaostahili kuhakikisha wamevipata vishikwambi hivyo. Si hivyo tu bali pia wahakikishe malalamiko haya hayapo na wasimamie kuona makundi yaliyopaswa kupewa yanafikiwa na wale ambao hawajapata wapate. Baada ya wiki moja tupate taarifa zoezi hili limekwendaje," alisisitiza.

Mjema alisema kutolewa kwa vishikwambi hivyo ni mwendelezo wa jitihada za serikali kuwawezesha na kuwajengea uwezo walimu kuwa na vitendea kazi na kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Katika kuendelea kuwawezesha walimu kuwa na vitendea kazi na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji, ilielezwa Septemba 15, mwaka jana, kwamba vishikwambi vilivyotumika wakati wa sensa ya watu na makazi Agosti 23, 2022 vitatagawiwa kwa walimu wote baada ya shughuli hiyo kumalizika.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Juma Kipanga, alisema vishikwambi vilivyotumika wakati wa sensa ya watu na makazi vilikuwa 6,600 kwa upande wa Zanzibar na 293,400 Tanzania Bara.

Pia alisema wizara hiyo imeongeza vishikwambi zaidi ya laki moja hivyo kufanya idadi hiyo kutosheleza.


## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**DUNSTAN RICHARD OMARI** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba: **TAE064892** iliyotolewa DAR ES SALAAM PCO mwaka 2018. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/27242/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TAMBA ANDREA WARENSE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAUM** yenye usajili namba **T257 DLD,** CHASSIS NAMBA: **NCZ200097910** na ENGINE NAMBA: **1NZC277629.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/28127/2023**

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**SUMMONS BEFORE THE COMMISSION FOR MEDIATION AND ARBITRATION**
**(HATI YA WITO MBELE YA TUME YA USULUH ISHI NA UAMUZI)**

**((made under Regulation 34(1) (imetengenezwa chini ya kanuni ya 34(1))**
**Labour Dispute( mgogoro wa kikazi Na.) CMA/DSM/TMK/300/202/91/2022**
**Between/ Baina ya**
**JUMAA KHASSIM KANIKA AND 10 OTHERS.......Applicant(Mlalamikaji/Mwombaji)**
**And/Na**
**TANGA FRESH LIMITED & HENRY AUCTION MART(2002) CO.........Respondent( Mlalamikiwa/Mjibu maombi)**
**NOTICE TO ATTEND MEDIATION/ARBITRATION HEARING**

**(TAARIFA YA KUITWA KUHUDHURIA KWENYE SHAURI LA USULUHISHI/UAMUZI)**

Take notice that the above mentioned Mediation/ Arbitration has been fixed for hearing on 25th day of JANUARY year 2023 at 10;00 hours at TEMEKE. (Unaarifiwa kuwa shauri lililotajwa hapo juu, linakuja kwa hatua ya usuluhishi/Uamuzi, Limepangwa kusikilizwa tarehe 25 mwezi 01 mwaka 2022, saa 4:00 mahali TEMEKE, karibu na uwanja wa Taifa).

You are required to appear before the Commission in person and or accompanied by an Advocate/ personal representative as instructed and produce on that day all relevant documents you intend to rely upon in support of your defence. You are further cautioned to remain in attendance until permitted by the commission ( unatakiwa kufika binafsi ama kwa kuambatana na wakili/mwakilishi wako mbele ya Tume kama ulivyoagizwa. Unapaswa kuleta vielelezo/nyaraka muhimu unazokusudia kuzitumia katika utetezi wako. Unatahadharishwa usipuuze kutii wito huu na unatakiwa kubakia kwenye majengo ya Tume mpaka utakapo ruhusiwa kuondoka na Tume).

Given under my hand and seal of the commission, this 14th day of Nov year 2022.( imetolewa na kugongwa muhuri wa Tume leo tarehe.....mwezi....mwaka, 2022)

COMPANY NUMBER 139438744

**THE COMPANIES ACT**
**(CAP 212 R.E. 2002)**
**CEMNKO LIMITED**
**BOARD RESOLUTION**

AT A DULLY CONVENED AND CONSTITUED SPECIAL RESOLUTION OF CEMNKO LIMITED HELD AT REGISTERED OFFICE OF THE COMPANPANY AT PLOT NO. 131 MKOMAZI STREET, MINAZINI, KURASINI, DAR ES SALAAM ON 9TH AUGUST 2022, AT 4:00 PM.

**PRESENT:**
1. CESEAR THERESA MLOKA....................................Director & Chairman
2. SITHANDILE KHABELA..........................................Director
3. JOSEPH NICAS LUKOA..........................................Director & Secretary

**AGENDA**
1. Voluntary winding up of Templars Limited
2. AOB

**OPENING**
The Chairman called the meeting to order at 4:00 PM

**DISCUSSION**
The chairman of the Board introduces the Agenda of Voluntary winding up of CEMNKO Limited. After long discussion the issue thoroughly, all, members of the Board agreed and resolved that indeed the company should be winded up voluntary.

**CLOSING**
In the absence of any further business, the Chairman closed the meeting at 4:38 PM

**CERTIFIED TRUE EXTRACT**
**(By Order of the Board)**

Dated at Dar es Salaam this 9th day of August 2022

CEMNKO LIMITED
P.O Box 42689
Dar es Salaam
Plot 131 Mkomazi Street
Kurasini

CESEAR THERESA MLOKA
**Chairman**

JOSEPH NICAS LUKOA
**Secretary**

217237102

## KILIO CHA SHULENI KIBORIANI...

# Madawati yapokewa, vyoo vinajengwa, madarasa na makazi ya walimu yaja

## -Neema yasogea hadi zahanati ya kijiji

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa** MPWAPWA





Picha elekezi ya madarasa na nyumba za walimu zinazotarajiwa kujengwa na serikali shuleni Kiboriani kukabili hali mbaya iliyothibitishwa baada ya kuripotiwa na gazeti hili. **PICHA: TAMISEMI**

AGOSTI mwaka jana, Nipashe iliripoti hali mbaya ya miundombinu na samani kwenye Shule ya Msingi Kiboriani wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma.

Ilishuhudiwa na Nipashe shuleni huko kuwapo uhaba wa walimu, madarasa, nyumba za walimu, madawati, ofisi, meza na viti kwa walimu huku vyoo vya wanafunzi vikiwa na uchakavu unaohatarisha usalama wa wanafunzi.

Shule hiyo ambayo kipindi hicho ilikuwa na jumla ya wanafunzi 420 (wasichana 227), haikuwa na mwalimu wa kike, hivyo kuwanyima fursa wanafunzi wa kike kupewa elimu rika na hata kupata huduma stahiki shuleni wanapokumbana na shida zinazohitaji utatuzi unaopaswa kufanywa na mwalimu wa kike shuleni.

Siku chache baada ya kuchapishwa kwa ripoti hiyo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alizuru Kiboriani na kuahidi serikali itajenga madarasa, nyumba za walimu na vyoo ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji shuleni.

Silinde aliyefuatana na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Sinyamule na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Mpwapwa, akikiri kuyashuhudia yaliyoripotiwa na Nipashe, akisema serikali mwaka huu wa fedha (2022/23) itatoa fedha kwa ajili ya kujenga vyumba viwili vya madarasa na nyumba moja ya walimu itakayokuwa na uwezo kwa kuhudumia familia tatu (3 in 1).

Naibu Waziri huyo pia aliwaomba wananchi wa Kijiji cha Kiboriani kushiriki uboreshaji wa miundombinu ya shule hiyo ili kuunga mkono jitihada za serikali.

### WACHUKUA HATUA

Baada ya miezi mitano, Nipashe inarejea tena Kiboriani kwa lengo la kuona utekelezaji wa yaliyoahidiwa na serikali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi Kiboriani, Isaya Chitema, anabainisha kuwa wamemaliza ujenzi wa shimo kwa ajili ya vyoo vya wanafunzi, mradi huo wakiutekeleza kwa kutumia Sh. milioni 2.3 zilizochangwa na wanakijiji wa Kiboriani (kila kaya ikitakiwa kuchangia Sh. 5,000).

Chitema anasema kuna fungu lingine limetolewa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa lengo la kufanikisha ujenzi wa vyoo shuleni Kiboriani (Sh. milioni nne kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, George Fuime).

Chitema anasema: "Tayari tumeshafunika shimo la choo, kinachofuata sasa ni kunyanyua ukuta kwa ajili ya vyoo vyenyewe, matofali tunayo. Tatizo la kukosa vyoo bora shuleni sasa linapata ufumbuzi."

Kwa mujibu wa Chitema, choo kipya kinachojengwa Kiboriani kitakuwa na matundu sita (matatu kwa ajili ya wasichana na mengine matatu kwa ajili ya kaka zao).

### MADAWATI

Kuhusu kikwazo cha uhaba wa madawati, Chitema anabainisha kuwa Jumatatu ya wiki hii alikabidhiwa madawati 21 na Kamati ya Mazingira ya Kijiji cha Kiboriani, hivyo shule hiyo kuwa na madawati mapya 33 yaliyotengenezwa hivi karibuni.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira ya Kijiji cha Kiboriani, Baraka Msurwa anafafanua namna madawati hayo yalivyopatikana, akitamka: "Kijiji kiliomba kibali TFS (Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania) ili kukata miti kwa ajili ya kutengeneza madawati. Kibali kilipotoka miezi minne iliyopita, Kamati ya Shule ilikubaliana na wazazi kila mzazi wa mwanafunzi atoe mchango wa Sh. 1,000.

"Fedha zilipopatikana, tukamlipa mfundi na kumnunulia mahitaji kwa ajili ya kutengeneza madawati, ndipo yakapatikana haya madawati 21."

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi Kiboriani, Chitema, anaendeleza ufafanuzi huo, akisema: "Madawati mengine 12 yametengenezwa kupitia mradi wa EK. Huu ni mradi wa shule yetu, wanafunzi walilima mahindi kwenye shamba la shule, mahindi yameuzwa zikapatikana fedha ambazo zimetumika kutengeneza madawati 12.

"Tunasubiri utekelezaji wa ahadi ya Serikali Kuu kuboresha mazingira ya shule. Tunaishukuru serikali kwa kuliezeka boma la zahanati yetu".

Zikirejewa takwimu za samani kwenye Shule ya Msingi Kiboriani, madawati 33 yaliyokabidhiwa kwa Kamati ya Shule Jumatatu, yanaifanya shule hiyo kuwa na jumla ya madawati 88, hivyo kupunguza uhaba uliokuwapo kutoka madawati 85 hadi 52.

Kwa mantiki hiyo, kwa sasa uwiano wa madawati na wanafunzi shuleni Kiboriani ni 1:4 (yaani dawati moja linatumiwa na wanafunzi wanne). Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inaelekeza kuwapo uwiano wa 1:3, yaani dawati moja litumiwe na wanafunzi watatu wa shule ya msingi.

### KAULI HALMASHAURI

Akizungumza na Nipashe kwa simu jana akiwa mjini Dodoma, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, George Fuime, alisema wanafuatilia kwa kina utatuzi wa kero zinazoikabili Shule ya Msingi Kiboriani na zingine zenye kero za aina hiyo kwenye eneo lake la uongozi.

"Wananchi wamefanya kazi kubwa madawati yamepatikana, ujenzi wa choo unaendelea. Juzi (Jumatano) tumeidhinishwa kwenye kikao cha baraza kupeleka Kiboriani Sh. milioni nne kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ili kuwezesha ujenzi wa vyoo.

"Pia Sh. milioni 50 zimetolewa kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Kiboriani," Fuime alisema na kubainisha kuwa hatua kubwa zaidi kuinusuru shule hiyo inatarajiwa kuchukuliwa na Serikali Kuu iliyoahidi kujenga nyumba za walimu na madarasa mapya katika mwaka huu wa fedha.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa vyoo shuleni Kiboriani juzi. Shule hiyo iliripotiwa na gazeti hili mnamo Agosti 7, mwaka jana kuwa na hali mbaya ya huduma hiyo pamoja na miundombinu ya madarasa, nyumba na ofisi za walimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Serikali imetenga Sh. trilioni 1.15 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi zenye uchakavu kupitia Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Awali na Msingi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Angellah Kairuki, alisema mjini Morogoro wiki iliyopita kuwa ukarabati huo unatarajiwa kufanyika kwa miezi miwili kuanzia mwezi huu.

Alisema baadhi ya shule zitavunjwa na kujengwa upya na nyingine zitafanyiwa ukarabati mkubwa na mdogo ili ziwe na mazingira bora kwa walimu na wanafunzi.

"Serikali inatambua shule nyingi ni za muda mrefu ambazo zilijengwa na wazee na nyingine kwa njia ya kujitolea na zimedumu kwa muda mrefu na imefika wakati wa kuziboresha, Angellah alisema.

Uamuzi huo wa serikali unajibu hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya Aprili 2017, alipofanya ukaguzi maalum wa miundombinu na samani za shule za msingi nchini na kubaini nyingi zina hali mbaya.

# Kigogo TUCTA adai mwekezaji kumpora ardhi

**Na Thobias Mwanakatwe**

KATIBU Mkuu mstaafu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Nicholas Mgaya, ameilalamikia kampuni ya kupasua mawe na kuuza kokoto ya Kitulwe Company Ltd (KCL) kwa madai ameingia kinyemela katika shamba lake na kuanza kufanya shughuli hiyo bila makubaliano yoyote.

Mgaya ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Misongeni, Kata ya Magila, Muheza mkoani Tanga, amepanga kumburuza mahakamani mwekezaji huyo na pia kuwasilisha malalamiko yake kwa Rais na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili mwekezaji huyo asimamishwe kuendelea na shughuli zake katika shamba hilo.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii jana, Mgaya alisema alichukua hatua ya barua kwa serikali ya kijiji cha Tingeni, Baraza la Ardhi la Kata ya Tingeni na Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kulalamikia suala hilo lakini hajajibiwa hata barua moja na mwekezaji anaendelea kufanya shughuli.

Mwekezaji huyo alipewa ardhi hiyo kuchimba mawe eneo la mlima wa Msagia - Ukoka katikati ya kijiji cha Tingeni Kata ya Tingeni na Kijiji cha Misongeni Kata ya Magila wilayani Muheza.

Alisema ardhi ya shamba lake iko kati ya kijiji cha Misongeni kata ya Magila na kijiji cha Tingeni kata ya Tingeni wilayani Muheza, hivyo mpaka upo katikati ya bonde lakini upande wa kijiji cha Tingeni, mwekezaji huyo ndiko anafanya shughuli zake zaidi za kupasua mawe kwa ajili ya kuuza kokoto.

Mgaya alisema mwekezaji huyo amepewa ardhi katika mazingira ya kutatanisha katika shamba lake na ameanza kufanya kazi bila kuwashirikisha wenye mashamba yao.

Alisema kama serikali haitachukua hatua za makusudi katika kutatua mgogoro huo wa ardhi, kuna hatari ya kutokea vurugu kwa kuwa wakazi wa kijiji hicho wamedai hawako tayari kuona mwekezaji anapora maeneo yao kinyemela na kuwafanya kuwa wakimbizi katika ardhi yao.

Mgaya alimwomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, kufika katika kijiji cha Misongeni ili kujionea hali halisi ya ardhi ya shamba lake ambayo mwekezaji analifanyia kazi bila kulipwa fidia.

Alisema mwekezaji huyo anaharibu ardhi ya mashamba ya watu kwa kuchimba migodi ya kupasua mawe kwa baruti ili kutengeneza kokoto mashamba yana mashimo hayafai hata kulima tena. "Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 kifungu cha tano ya mwaka 1999 inasema halmashauri ya kijiji haitagawa ardhi au kutoa hatimiliki ya kimila bila kwanza kupata idhini ya mkutano wa kijiji. Kifungu cha sita cha sheria hiyo kinaeleza Halmashauri ya Kijiji italazimika kutoa taarifa na kuzingatia maoni ya mkutano wa kijiji kuhusu uendeshaji na usimamizi wa ardhi ya kijiji. Yote hayo hayajazingatiwa," alisema.

Msimamizi Mkuu wa Kitulwe Company Ltd, Albert Shembilu, alisema kampuni hiyo iko kihalali katika eneo hilo na ina vibali vyote vya kufanyia kazi kutoka Wizara ya Madini.

Alisema tayari kampuni hiyo imeshawalipa fedha wananchi ambao wana mashamba yao na kwamba hakuna hata mwananchi mwenye eneo lake la ardhi ya shamba wanapofanya kazi hajalipwa haki zake.

"Wote tuliochukua maeneo yao hapa tulishawalipa na kampuni imetoa ajira na inaingiza kipato kwa kulipa kodi kwa serikali, wilaya na kijiji," alisema.



Katibu Mkuu mstaafu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Nicholas Mgaya ambaye Mkazi wa Kijiji cha Misongeni, Kata ya Magila, wilayani Muheza, mkoani Tanga, akionyesha mashimo katika moja ya mashamba yake ambayo mwekezaji wa kampuni ya kupasua mawe na kuuza kokoto ya Kitulwe Company Ltd (KCL) anadaiwa kuingia kinyemela na kufanya shughuli ya kupasua kokoto. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Jamhuri yafunga ushahidi wa kesi waliodai ni TISS

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa mashtaka katika kesi ya tuhuma za kujifanya maofisa wa Idara ya Usalama wa Taifa (TISS) katika ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, inayowakabili wafanyabiashara wawili, umefunga ushahidi kwa mashahidi wanne.

Wafanyabiashara hao ni Joshua Jeremia (37) na Yahya Abdallah (31) ambao wanashtakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa mashtaka mawili ya kujitambulisha kuwa ni maofisa wa TISS.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Timotheo Mmari, alitoa taarifa ya kufunga ushahidi huo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate, baada ya shahidi namba nne, Sudi Mwashitete, kumaliza kutoa ushahidi wake.

"Mheshimiwa hakimu tunaomba kufunga kesi kwa upande wetu, shahidi huyu ndiye wa mwisho, hakuna shahidi mwingine tutakayemleta," alidai Mmari.

Baada ya ombi hilo, Hakimu Kabate aliahirisha kesi hiyo hadi Februari 21, mwaka huu, kwa ajili ya uamuzi kama washtakiwa wana kesi ya kujibu au la.

Wakati akitoa ushahidi wake, Mwashitete alidai kuwa yeye ndiye aliwakamata washtakiwa hao kwenye korido ya ofisi ya DPP Mwakitalu, baada ya kuthibitishiwa kuwa ndiyo watuhumiwa waliyojitambulisha kuwa wao ni TISS.

Alidai kuwa aliandika barua ya Septemba 13, 2022 kwa Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa ili kujua kama kweli washtakiwa ni watumishi katika idara yake.

Mwashitete alidai Septemba 21, 2022 walipata majibu kutoka ofisi ya Katibu Mkuu Ikulu kuwa washtakiwa hao si maofisa wa TISS na hawako katika orodha ya malipo ya wafanyabiashara.

Awali, DPP Mwakitalu aliieleza mahakama watu wawili waliyojitambulisha kwake kuwa ni maofisa wa TISS ili asitishe majadiliano ya kumaliza kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Herbender Seth na wenzake.

Aidai kuwa washtakiwa hao walitenda makosa hayo Juni 12, 2022 katika ofisi za DPP zilizoko katika jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Dar es Salaam.

Ilidaiwa kwamba washtakiwa hao walijitambulisha kwa DPP Mwakitalu na Naibu DPP Joseph Pande kwamba wao ni maofisa kutoka TISS.

Washtakiwa wote wako nje kwa dhamana, baada ya kutimiza masharti ya kuwa na wadhamini wawili wa kuaminika kwa kila mshtakiwa waliotia saini bondi ya Sh. milioni saba.

# Hatima ya ushiriki ACT katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa leo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI Kuu ya Chama Cha ACT-Wazalendo, inakutana leo jijini Dar es Salaam, pamoja na mambo mengine, itajadili na kutoa msimamo juu ya hatima yake katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) Zanzibar.

Hatua hiyo inatokana na awali kupinga uteuzi wa Thabit Idarous Faina mwishoni mwa mwaka jana kuwa Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

Kabla ya kujilikana kwa hatima hiyo leo, vikao mbalimbali vya chama hicho kwa upande wa Zanzibar viliamua kukusanya maoni ya wananchi baada ya uteuzi Faina anayedaiwa kuhusika na matokeo yote ya uchaguzi wa Zanzibar wa mwaka 2020.

Matokeo hayo yalizua sintofahamu kwa wafuasi na wanachama wa ACT-Wazalendo kabla ya kurudi katika meza ya majadiliano na kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Taarifa ya chama hicho iliyosambazwa Januari 16, mwaka huu na kutiwa saini na Janeth Rithe, Naibu Katibu wa Habari Uenezi na Mawasiliano kwa Umma, Janeth Rithe, ilisema Kamati Kuu inayokutana leo, mbali na kujadili hatima ya chama hicho katika SUK Zanzibar pia itajadili hali ya kisiasa nchini na kupokea mpango wa kujenga chama kwa mwaka 2023.

"Kamati kuu itajadili hali ya kisiasa ikiwa ni pamoja na hatua iliyofikiwa katika ajenda ya mabadiliko ya siasa nchini na kupitisha ratiba ya uzinduzi wa mikutano ya hadhara ya ACT-Wazalendo itakayofanyika nchi nzima," ilisema taarifa hiyo.

Akizungumza jana katika makao makuu ya chama hicho, Katibu Mkuu wa ACT- Wazalendo, Ado Shaibu, alisema baada ya Uteuzi wa Faina, kamati maalum ya Kamati Kuu ya ACT-Wazalendo Zanzibar, ilikutana kwa dharura na kukubaliana kuchukua maoni ya wananchi kabla ya kufikia uamuzi wa mwisho wa hatima ya ushiriki wake katika SUK.

"Wananchi walitoa maoni mbalimbali ambayo viongozi wetu waliyakusanya wakayachakata na sasa yatafikishwa katika Kamati Kuu hii kujadiliwa na kutolewa uamuzi.

"Sisi chama chetu tunafanya kila jambo lenye maslahi ya wananchi kwa ridhaa yao," alisema Shaibu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mashindano ya riadha ya wanawake mwanga mpya

**BARAZA** la Michezo la Taifa (BMT), limeandaa mashindano maalumu ya riadha ya wanawake yatakayofanyika leo na kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mashindano hayo yamepewa jina la Ladies First yanatarajiwa kushirikisha wanariadha wa kike zaidi ya 200 kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mashindano hayo yanayofanyika kwa msimu wa nne.

BMT imesema hadi kufikia jana jioni, mikoa 31 ilithibitisha kushiriki mashindano hayo na wanariadha wake walikuwa wameshawasili Dar es Salaam tayari kwa kushindana.

Wanariadha hao watachuana katika mbio za umbali wa kuanzia mita 100, 200, 400, 800 na mita 1,500. Pia watachuana katika kurusha vitufe. Mashindano hayo yameandaliwa kwa lengo la kuwapa nafasi wanariadha wa kike kuendeleza vipaji vyao na kuibua vipaji vipya vitakavyopatikana.

Ili kuwa na wachezaji wazuri, ni lazima kuwapo na mashindano ambayo yatawapima wachezaji husika na kwa kuanzia hapo, ndipo mwanzo wa kuwaandaa kwa kufuata misingi sahihi ya mchezo husika kuchukua nafasi yake.

Tukumbuke wanariadha au wachezaji wanaofanya vizuri katika mashindano mbalimbali duniani wanatokana na michuano kama hii ambayo huwa ni kama daraja la kuwapata wachezaji nyota na baadaye kupelekwa katika mafunzo kwa ajili ya kuendelezwa.

Tukumbuke miaka ya nyuma, wanamichezo walipatikana kupitia mashindano ya UMISETA na UMITASHUMTA, lakini sasa dunia imebadilika na serikali kwa kushirikiana na vyama vya michezo, wamekuwa wakiandaa mashindano ya ngazi mbalimbali ili kuendelea kusaka vipaji, kwa sababu inahitaji kuwekeza kuanzia ngazi ya chini.

Ni wazi makocha kutoka katika klabu mbalimbali watakaofika kushuhudia mashindano hayo, watapata nafasi ya kutambua vipaji vipya na kuwachukua ili kuwaandaa na michuano mbalimbali ya kitaifa na baadaye kimataifa.

Unaweza kusema kama Tanzania ilichelewa, lakini tukumbuke wakati sahihi ni wakati wa Mungu, huu ni msimu wa nne wa mashindano hayo, tunaamini makocha wanaendelea kupata wachezaji na kuwaandaa kwa malengo ya kushiriki michuano ya kimataifa na kuliletea taifa heshima.

Ili kufikia malengo ya kuwajenga wanamichezo wetu, tunaikumbusha serikali kupitia BMT isiishie kwa mchezo wa riadha pekee, iangalie na michezo mingine ambayo kwa hakika inashindwa kufanya vizuri kwa sababu wachezaji wake wanakosa maandalizi sahihi, michezo hiyo inakosa udhamini.

Kama ambavyo serikali iliwekeza nguvu zake katika mpira wa miguu wa wanawake na hatimaye mwaka jana timu ya wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), ilifanikiwa kufuzu kushiriki Fainali za Kombe la Dunia huko India, basi itupie jicho kwa michezo yote na kwa kufanya hivyo, itarajie kuvuna makombe mbalimbali.

Katika kuonyesha serikali imedhamiria, wasichana hao hawatashiriki michezo peke yake, watashiriki semina ya mafunzo ya kujitambua kiafya na kujiepusha na mimba za utotoni. Hii itawasaidia wachezaji kujiweka katika mazingira salama kwa sababu kupitia michezo, wanakutana na changamoto mbalimbali.

Tunaamini uwekezaji imara, huzaa matunda bora, hongera BMT, hongera serikali kwa kukumbuka kuendeleza wachezaji kuanzia ngazi ya chini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

### Kifo mchezaji Singida BS kiwaamshe waamuzi Bara

**JANUARI** 19, mwaka huu, tasnia ya michezo ilipatwa na mshtuko mkubwa baada ya kupata taarifa ya kifo cha mchezaji, Mohamed Banda, wa Singida Big Stars ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na klabu hiyo ilisema Banda ambaye alikuwa ni nahodha wa timu ya vijana wa umri chini ya miaka 17, alifariki dunia baada ya kugongana na kichwani na mchezaji mwenzake wakiwa katika mazoezi kwenye Uwanja wa Magereza uliopo mkoani Singida.

Baada ya kugongana zilifanyika juhudi za kuokoa maisha ya mchezaji huyo, ikiwa ni pamoja na kumwahisha katika Hospitali ya Mkoa, lakini alipoteza maisha baada ya kufikishwa.

Ni pigo kubwa kwa familia yote ya soka nchini na hasa tukikumbuka kuwa mara kwa mara huwa tunasikia taarifa za wachezaji wa nje ya nchi walifariki dunia wakiwa uwanjani.

Sitaki kuwaorodhesha hapa kwa sababu ni wengi, lakini baadhi yao walifariki kwa kuanguka wenyewe uwanjani kwa kile kinachoelezwa siku zote huwa ni mshtuko wa moyo.

Ukiacha hilo, wapo wachezaji wachache wanaopoteza maisha kutokana na kugongana na mchezaji wenzake uwanjani.

Kwanza kabisa nipende kuchukua fursa hii kuipa pole Singida Big Stars, mashabiki wa soka wa Singida, ndugu jamaa na marafiki, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), wapenzi na wadau wote wa mchezo wa kandanda hapa nchini.

Kwa kawaida tu watu wanauchukulia poa mchezo wa mpira wa miguu, ambapo wanauona ni mchezo salama sana tofauti na ngumi, mieleka, mbio za magari au pikipiki.

Lakini ukweli soka ni moja ya mchezo hatari sana ambao unaweza kuchukua maisha ya mchezaji muda wowote ule.

Ndiyo maana wakati wa mechi kunakuwa na watu wa huduma ya kwanza, madaktari na magari ya kubebea wagonjwa.

Hivi karibuni kulikuwa na mgogoro wa kanuni za magari ya wagonjwa, ambapo iliwekwa bila gari la kubebea wagonjwa, mechi haiwezi kuchezwa.

Wapo watu waliokuwa wanalichukulia kama jambo hili ni jepesi au halina msingi, yaani mechi isichezwe kwa sababu hakuna gari la wagonjwa?

Ni kwa sababu kila siku wanaona mechi zinaisha bila ya kuwa na matatizo yoyote.

Majeruhi wanakuwa ni wale wa kawaida tu.

Siku likitokea tatizo kama lililompata Banda ndiyo watu wanaanza kuona kumbe mpira wa miguu ni moja kati ya michezo hatari duniani.

Ni kweli, mpira wa miguu, pamoja na akili unatumia zaidi nguvu. Ndiyo maana kama wachezaji wanasukumana miili kwa miili, mwamuzi hapulizi filimbi. Kwa sababu hapo inayotumika ni fiziki na mwenye fikizi nzuri na kutumia akili zaidi ya mwenzake ndiye atakayeuchukua mpira.

Wakati mwingine inatokea bahati mbaya, wachezaji wanafanyiana rafu zisizokusudiwa na kuumizana, hata kusababisha kifo kabisa kama tulivyoona kwa Banda. Hiyo hutokea na nadra ni bahati mbaya sana.

Kwenye mpira huo huo wa miguu kuna baadhi ya wachezaji ambao wanakosa nidhamu na kuanza kuwachezea vibaya wenzao vibaya kwa makusudi.

Hao ni wale ambao wanazidiwa maarifa, ujuzi, vipaji na wenzao, hivyo wanaona njia pekee ni kuwachezea vibaya, kuwaumiza na kuwakatishia ndoto zao za kuendelea kucheza soka, au hata kusababisha ulemavu au kifo.

Badala ya kumpokonya mwenzake mpira kwa kutumia maarifa na nguvu zinazohitajika, mchezaji wanaruka kama wanacheza kareti na kumkanyaga mwenzake, au kupiga kichwa kwa nyuma na rafu nyingine zisizo na kichwa wala miguu.

Rafu za aina hii tunaziona na sasa zimekuwa nyingi sana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na waamuzi wengi wanaonekana waoga kuchukua hatua.

Tunawaomba waamuzi sasa, wawe wanachukua hatua stahiki kwa wachezaji wakorofi, wasio na nidhamu ya uchezaji uwanjani ili kulinda wale wanaoleta burudani na kuonyesha uwezo wao uwanjani.

## Shule Bora yaongeza uandikishaji wanafunzi

**Na Devota Mwachang'a,** KASULU

MRADI wa Shule Bora umesaidia kuhamasisha wazazi na jamii kupeleka watoto shuleni na kufanya uandikishaji kwa watoto wa darasa la kwanza mkoani Kigoma kuongezeka hadi asilimia 85 mwaka huu.

Hayo yalithibitishwa na Katibu Tawala Msaidizi (Elimu) Mkoa wa Kigoma, Paulina Ndigeza, wakati wa mkutano wa uhamasishaji wa Programu ya Shule Bora uliondaliwa na Cambridge Education Tanzania kwa wasimamizi wa vyombo vya habari na wahariri mkoani Kigoma uliofanyika mjini hapa.

Shule Bora ni mradi bunifu wa elimu wa serikali kwa ufadhili wa serikali ya Uingereza kupitia mfuko wa UK Aid unaotekelezwa katika mikoa tisa Tanzania Bara kwa kupokea utaalamu wa kiufundi kutoka Cambridge Education Tanzania, ikishirikiana na mashirika ya ADD International, International Rescue Committee na Plan International.

"Serikali na wadau wa elimu walifanya utafiti na kubaini changamoto za elimu mkoani kwetu. Mradi huu umekuja wakati sahihi na kuanza kuleta mabadiliko. Wazazi wameandikishaji watoto na sasa tumefikia lengo la kitaifa kwa kuandikisha watoto 67,900 kuingia darasa la kwanza na zaidi ya watoto 70,000 shule ya awali," alisema.

Aidha, Ndigeza alisema mradi wa Shule Bora umesaidia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia wanafunzi ambayo awali yalikuwa hafifu, pia umewezesha jamii kushiriki mikakati ya kuinua ubora wa elimu kwenye mkoa wao. Ofisa Elimu Taaluma Mkoa wa Kigoma, David Mwamalasi, alisema shule ni mali ya jamii, hivyo mradi huo umezingatia uhusiano kati ya wazazi na walimu (parents teachers partnership - PTP) kwa lengo la kuhakikisha wazazi wanatambua wajibu wao wa kuwalea watoto kitaaluma.

"Ili mtoto afanye vyema lazima uwepo ushirikiano baina ya mzazi na mwalimu. Wazazi wana mchango mkubwa katika kuhakikisha usalama wa watoto, hivyo wana jukumu la kuwahimiza watoto kwenda shuleni ili kuwaondoa kwenye mazingira yanayoweza kuchangia kuwa watoro na kupata mimba za utotoni," alisisitiza Mwamalasi.

Naye Meneja Mawasiliano wa Programu kutoka Cambridge Education Tanzania, Raymond Kanyambo, alisema lengo la mradi ni kuhakikisha elimu inapatikana kwa wote wanaostahili kuanzia elimu ya awali hadi sekondari na kuondoa ubaguzi wa aina yoyote kwa watoto kupata elimu.

Alibainisha maeneo makuu ya mradi huo kuwa ni pamoja na ufundishaji kwa kuonyesha namna wanafunzi wanajifunza, ujifunzaji kwa kuhakikisha wanafunzi wanajifunza kwa kadri inavyotakiwa na ujumuishaji kwa makundi ya watoto wote wa kiume, kike na wenye ulemavu. Mratibu wa Programu mkoani Kigoma, Celestine Bukango, alitoa tathmini ya utekelezwaji wa mradi wa shule bora wa mwaka uliopita akibainisha kuwa walimu wameongezewa uwezo wa ufundishaji jumuishi na kuzingatia usalama wa mtoto.

"Pia mafunzo ya kuwezesha mpango endelevu wa walimu kazini (MEWAKA) katika halmashauri za Kigoma Manispaa, Buhigwe, Kasulu Vijijini na Kakonko yamefanyika," alisema.

Mradi wa Shule Bora unatekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), unafanya kazi moja kwa moja na mamlaka za serikali za mikoa na halmashauri katika mikoa tisa yenye changamoto za kielimu. Mikoa hiyo ni Kigoma, Katavi, Rukwa, Dodoma, Mara, Singida, Simiyu, Tanga na Pwani.




Meneja Masoko na Mawasiliano wa Kampuni ya GF Trucks & Equipment's Ltd, Smart Deusi (kulia), akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, kuhusu maandalizi ya mkutano mkuu wa Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TATOA), utakaojadili changamoto mbalimbali jijini humo. Kushoto ni Mwenyekiti wa TATOA, Elias Lukumay na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Double Luck Consulting LTD, Sandeep Basra. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## JKCI kupima magonjwa ya moyo Zanzibar

**Na Joseph Mwendapole**

WATAALAMU wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kushirikiana na wenzao wa Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja Zanzibar, wanatarajia kufanya upimaji na matibabu ya moyo kwa wananchi wa Visiwa vya Zanzibar.

Upimaji huo utafanyika kwa watoto na watu wazima kwa siku tano mfululizo kuanzia tarehe 23 hadi tarehe 27 mwezi huu kuanzia saa mbili kamili asubuhi mpaka jioni katika Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja.

"Tutakuwa na wataalamu wa lishe ambao watatoa elimu ya lishe bora ambayo itawapa wananchi uelewa na kufuata mtindo bora wa maisha ambao utawasaidia kuepukana na magonjwa ya moyo," ilibainisha taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano JKCI, Anna Nkinda.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, magonjwa ya moyo ni miongoni mwa magonjwa yasiyoambukiza na yanaweza kuepukika kwa kufuata ushauri wa kitaalamu ikiwamo lishe bora na mazoezi.

Kupitia taarifa yake hiyo, Anna alisema watakaogundulika kuwa na matatizo ya moyo, watafanyiwa uchunguzi zaidi na kupatiwa matibabu hapohapo au kupewa rufani kwenda kutibiwa kwenye Taasisi ya JKCI Muhimbili, Dar es Salaam.

"Tunawaomba wananchi wajitokeze kwa wingi kupima afya zao kujua kama wana matatizo ya moyo ili kuanza matibabu mapema kwa atakayebainika kuwa na maradhi ya moyo," alisema.

Katika kutoa huduma ya matibabu ya moyo kwa kuwafuata wananchi mahali walipo kwa mwaka 2022, Anna alibainisha kuwa JKCI ilifanya upimaji na matibabu ya moyo kwa watoto na watu wazima katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Geita, Mtwara na Lindi na kuwahudumia watu 3,935.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kati yao, 1,391 walikuwa na magonjwa mbalimbali ya moyo ikiwamo shinikizo la damu, kutanuka kwa misuli ya moyo, kuziba kwa mishipa ya damu ya moyo, matundu ya moyo hasa kwa watoto na valvu za moyo zilizoharibika.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa wagonjwa 335 walipewa rufani kwenda kupata matibabu JKCI ambako walipata matibabu.

AINA ZA MAGONJWA

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa magonjwa ya moyo yanajumuisha ugonjwa wa moyo unaotokana na kuathirika kwa mishipa ya damu (Coronary artery disease), watu wengi wanaopata shida hiyo, mishipa ya damu hupasuka na kuharibika hutokana na mishipa ya damu kuwa na uchafu na mafuta mengi na kufanya damu isipite vizuri.

Mapigo ya moyo kwenda tofauti, shida ambayo hutokea pale mapigo ya moyo yanapokwenda taratibu isivyo kawaida au kwenda haraka isivyo kawaida, pia mapigo ya moyo kwenda ovyo hali ambayo ni hatari na huua watu wengi.

Moyo kushindwa kufanya kazi (Heart Failure) ambayo ni moyo hushindwa kufanya kazi yake kama kusukuma na kusambaza damu, kusambaza oksijeni na hali hiyo inatokea kwa mtu mwenye magonjwa kama ugonjwa wa moyo wa mishipa kuathirika, shinikizo la damu, na magonjwa mengine.

Magonjwa ya moyo ya kuzaliwa (Congenital heart disease) ambayo ni magonjwa ambayo wengi huzaliwa nayo, yanaweza kuwa ni baadhi ya kasoro katika mwili kama baadhi ya chemba za moyo kuziba au kupasuka, oksijeni kupita kwa shida na vinginevyo.

## RC ataka sheria ndogo ya kudhibiti mifugo mitaani

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kutunga sheria ndogo itakayotumika kuzuia mifugo inayozurura ovyo mitaani na kufanya uharibifu wa mazao na miti iliyopandwa.

Alitoa agizo hilo juzi alipoisikiliza kero za wananchi wa Iramba ambao pamoja na mambo mengine, walilalamika kuhusu mbuzi wanaozurura mitaani na kuharibu miti na mazao mengine yaliyopandwa.

Serukamba alimwagiza Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Iramba, Huseni Sepoko, kuhakikisha katika kipindi kifupi wawe wametunga sheria ndogo ambazo zitawasaidia kuzuia wanyama wanaorandaranda mitaani kwa kuikamata mifugo hiyo na kuwapiga faini wamiliki wake.

"Mkurugenzi hakikisheni katika kipindi kifupi kijacho, mtunge sheria ndogo ambazo zitazuia mifugo kuzurura mitaani na sheria hiyo iwe na nguvu ya kutoa adhabu kali kwa watakaokiuka utaratibu," alisema.

Aliongeza kuwa kwa sasa ni mpango wa mkoa kuhakikisha kunapandwa miti zaidi ya milioni tatu na kuifanya Singida kuwa mji wa kijani, jambo ambalo haliwezi kufanikiwa ikiwa miti hiyo itaendelea kuharibiwa na mbuzi wanaozurura mitaani.

Aliwataka viongozi wa halmashauri hiyo kuhakikisha wanawafuata wananchi walipo na kutatua kero zao badala ya kukaa ofisini kusubiri viongozi wa ngazi ya juu wanapotoka na kila mtumishi ahakikishe anakamilisha majukumu yake kwa wakati.

Alisema wananchi hao wanatarajia kusaidiwa changamoto walizonazo ambazo sio kubwa lakini wao wamekuwa wakitumia muda mwingi kwenda kusimamia masuala ya kujenga barabara na madarasa na kuyaweka kanda matatizo yanayowahusu wananchi.

"Mimi ninaamini watu hawa ambao changamoto zao hamzifanyii kazi ndio waliyoiweka serikali iliyoko madarakani, hivyo wangetamani kuona inatatua matatizo yao kupitia sisi tuliopewa dhamana ya kufanya hivyo baada ya kupewa kufanya kazi ya kuwatumikia," alisema.

Serukamba aliwaomba viongozi na watumishi wa wilaya hiyo kubadilisha mfumo wa kufanya kazi kwa mazoea badala yake uwe wa kutatua changamoto za wananchi.

Aliwataka wafanyakazi wa halmashauri hiyo kujiuliza wanapokwenda kazini kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa wamefanya nini na wamewahudumia kina nani na akaomba wawe na lugha nzuri kwa wanaowatumikia.

Serukamba pia aliiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kuhakikisha inaondoa taka zote zilizoko kwenye maguba yaliyoko kwenye makazi ya watu na maeneo mengine.

Akiwa katika ziara hiyo, Mkuu wa Mkoa alisikiliza jumla ya kero 32 zikiwamo za ardhi, maji na madeni na usafi wa mazingira.

# DC apiga 'stop' uingizaji holela mifugo

**Na Steven William,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, amepiga marufuku uingizwaji holela wa mifugo wilayani hapo na kuahidi kuanzisha operesheni maalum kijiji kwa kijiji kuwaondoa wafugaji waliovamia maeneo hayo kutoka nje.

Moyo alitoa agizo hilo juzi katika mkutano wake na wafugaji uliolenga kujadiliana namna ya kuboresha shughuli za ufugaji na kuondosha migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikisababishwa na uvamizi wa mashamba kutoka kwa wafugaji.

Alisema kuna madai kwamba baadhi ya viongozi wa serikali za vijiji wamekuwa na tabia ya kuwapokea kinyemela wafugaji kutoka maeneo mbalimbali nje ya Wilaya ya Iringa.

Mkuu huyyo wa wilaya alisema serikali haiko tayari kuwafumbia macho viongozi wa namna hiyo wanaokiuka maadili ya uongozi na kwamba watakaobainika kuruhusu mifugo kuingia katika vijiji vyao, watawajibishwa kwa mujibu wa sheria. Alisema viongozi hao kwa kiwango kikubwa wamekuwa wakichochea ongezeko la migogoro baina ya wafugaji na wakulima.

Kupitia risala ya wafugaji, Moyo alipokea malalamiko kadhaa vikiwamo vitendo vya urasimu vinavyofanywa na baadhi ya viongozi wa vijiji ikiwamo kupora maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za ufugaji na kuyabadilisha matumizi hali inasababisha wafugaji kukosa maeneo ya malisho.

Hali hiyo, alisema inawafanya wafugaji kulisha mifugo yao katika maeneo yasiyo rasmi, hivyo kuibua migogoro ya mara kwa mara. Mwenyekiti wa Umoja wa Wafugaji Wilaya ya Iringa, Emmanuel Sailutye, alizitaja changamoto zingine ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutokuwa na sera ya kutambua maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji, utozaji holela wa faini kwa makosa ya kuingia katika maeneo yasiyoruhusiwa, upanuzi wa mipaka ya hifadhi na kuanzishwa kwa hifadhi ya jamii hatua inayofanya wafugaji kukosa maeneo ya malisho.

Kutokana na malalamiko hayo, Moyo alimwagiza Mkuu wa Idara ya Ardhi Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, kuwasilisha taarifa ya mpango wa matumizi bora ya ardhi wa kila kijiji ili serikali ichukua hatua endapo kuna viongozi waliobadili matumizi ya maeneo kinyume cha utaratibu.

Moyo aliwataka wafugaji kuwa watulivu wakati serikali ikiendelea kushughulikia malalamiko na maombi yaliyotolewa na wafugaji hao.

Katika mkutano huo, ofisa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Iringa, Anneth Mwakatobe, aliwasihi wafugaji kujiepusha na vitendo vya rushwa huku akiwataka kutoa taarifa pindi wanapoombwa rushwa na viongozi na watu wanaowarubuni kuwa watawasaidia wanapokumbana na changamoto katika shughuli zao.

Alisema serikali iko macho kushughulikia changamoto zote zinazowakabili wananchi wake, hivyo kutoka au kupokea rushwa ni ukiukwaji wa mikakati ya utoaji huduma kwa wananchi.



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, akipanda mti wakati wa uzinduzi wa upandaji miti kiwilaya katika kijiji cha Magubike na Sekondari ya Dimitrios, Kata ya Nzihi juzi, ambapo lengo ni kupanda miti milioni 1.5. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## DED aagizwa ukarabati wa kituo cha afya

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Chalinze, Bagamoyo mkoani Pwani, Hassan Mwinyikondo, amemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kufanya ukarabati wa dharura kwenye kituo cha afya Chalinze.

Mwinyikondo alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea kituo hicho akiwa ameambatana na baadhi ya madiwani na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Ramadhani Possi.

"Agizo langu kwako mkurugenzi ukarabati uanze ndani ya wiki mbili tuma wataalamu wako wafanye tathmini hiki kituo ndio kiko barabarani kinasaidia wengi kwa uchakavu huu hatuwezi kuendelea kuwa kimya," alisema Mwinyikondo.

Naye Possi alisema amepokea maelekezo hayo na anaenda kufanyia kazi kwa kutuma wataalamu wa kufanya tathmini na ukarabati utaanza ndani ya wiki moja.

Possi alisema maagizo hayo yatafanyiwa kazi kwa haraka kutokana na umuhimu wa kituo hicho ambacho kinahudumia wakazi wengi wa Chalinze na kutokana na kuwa eneo la barabarani wapo watumiaji wanatoka nje ya mji huo.

Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Dk. Isdory Mfugale, alisema hali ya baadhi ya majengo ya kituo hicho hayako katika hali nzuri kutokana na uchakavu.

Aidha, alisema majengo mengi ni ya muda mrefu na hayajafanyiwa ukarabati na hivyo kutokana na uchakavu uliopo baadhi ya majengo hayatumiki na hivyo kuhitaji ukarabati wa haraka.

# Mkandarasi aeleza chanzo kusuasua ujenzi wa soko

**Na Joseph Mwendapole**

MKANDARASI Kampuni ya Namis Corporate Ltd anayejenga soko la Tandale, ameelezea changamoto za kutokamilika kwa wakati kwa soko hilo ikiwamo kutokulipwa kwa wakati.

Msimamizi wa mradi huo, James Msumari, alisema juzi kuwa walianza mradi huo Septemba 14, 2019 bila kupata malipo ya awali kwa ajili ya ujenzi huo na badala yake zililipwa miezi 10 baada ya ujenzi kuanza.

Alisema ucheleweshwaji wa malipo uliendelea pia kwa malipo yaliyofuata na kwamba ambapo hali hiyo ilikuwa ikifanyika kwa miezi mitatu hadi saba.

Msumari alisema baada ya kuanza kwa ujenzi huo, walikutana pia na changamoto kadhaa wa kadha ikiwamo maongezeko ya kazi ambazo hazikuwa kwenye mkataba.

Alitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni kulazimika kujenga soko la dharura kwa ajili ya kuwahamisha wafanyabiashara waliokuwa kwenye soko hilo ili kuwezesha ujenzi kuanza kwa wakati.

"Tulilazimika kujenga soko la dharura jambo ambalo halikuwamo kwenye mkataba na hiyo tulifanikiwa hatimaye tukaanza ujenzi lakini gharama hizo hazikuwa kwenye mkataba wetu," alisema.

Msumari alisema ufinyu wa eneo la ujenzi nao umechangia kwa kiwango kikubwa kuchelewa kukamilika kwa mradi huo kwa kuwa wanalazimika kuweka vifaa vingi vya ujenzi nje ya eneo la mradi.

"Lile eneo ni finyu sana na wakati mwingine unaleta mzigo mkubwa unaweka mbali na 'site' (sehemu ya ujenzi) kisha unaupeleka kidogo kidogo. Na hata ujenzi tunalazimika kuufanya kwa awamu ili kuhifadhi baadhi ya malighafi kwenye eneo hilo," alisema.

Alisema wanalazimika kuchanganya zege la ujenzi sehemu nyingine na kisha kulisafirisha kwenda eneo hilo kutokana na ufinyu wa nafasi kwenye eneo la ujenzi.

Pamoja na changamoto hizo, alisema ujenzi huo umefikia asilimia 80 na kwamba ingawa manispaa iliwataka wakabidhi Novemba, mwaka jana, waliomba wakabidhi Juni, mwaka huu, na kwamba wana uhakika watakamilisha ujenzi katika muda uliopangwa.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alitembelea soko hilo juzi kuangalia maendeleo ya ujenzi wake na kumtaka mkandarasi huyo kuongeza kasi ya ujenzi.

Makalla alisema tayari serikali ilishamlipa mkandarasi huyo shilingi bilioni saba kati ya 10 anazodai hivyo alimtaka aongeze idadi ya mafundi ili kukamilisha haraka mradi huo.

"Nyinyi ni kampuni kubwa sana na mmeshalipwa shilingi bilioni saba kati ya shilingi bilioni 10, soko lilipaswa kukamilika mwaka 2020 lakini mmeomba kuongezewa muda wa mkataba mpaka Juni mwaka huu, nawaagiza mwongeze mafundi na kazi zifanyike kila siku ili soko likamilike, " aliagiza Makalla.



HABARI DODOMA

# Kizimbani madai hasara bil. 264/-

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa mkoani Dodoma (TAKUKURU) imewafikisha mahakamani watu sita kwa kuisababishia hasara ya Sh. milioni 264.5 Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino.

Waliofikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma mbele ya Hakimu Janeth Musaroche ni pamoja na Mkurugenzi wa Kampuni ya Joroji Construction Ltd, John Bahem, Heri Mwafute, George Mwakamele, Seleman Msafiri, Shaban Mpwepwe na Noel Lukuwi.

Watu hao walikuwa wajumbe wa kamati ya tathmini ya halmashauri hiyo kwenye zabuni ya kutengeneza miundombinu ya maji katika kijiji cha Manzase mwaka 2013.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Takukuru Dodoma, Sosthenes Kibwengo, watuhumiwa hao walisomewa makosa sita ikiwamo uhujumu uchumi ambalo ni kinyume na kifungu cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa.

Alisema makosa mengine ni kumdanganya mwajiri, kutumia madaraka vibaya kujinufaisha na kutumia nyaraka za serikali kufanya udanganyifu.

Alifafanua kuwa watuhumiwa hao walitenda kosa hilo 2013 ambapo taasisi hiyo ilifanya uchunguzi na kubaini hasara hiyo.

"Takukuru kwa kushirikiana na Ofisi ya Mashtaka ya Taifa iliwasilisha shauri hilo mahakamani ili watuhumiwa wakajieleze," alisema.

Aliitaka jamii kuendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi hiyo ili kuwabaini waharibifu wa miradi ya maendeleo hapa nchini.

# Maofisa ununuzi serikali kikaangoni madai utendaji wa kazi usioridhisha

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MAOFISA ununuzi 68 kati ya 73 kutoka taasisi mbalimbali za serikali wametakiwa kuwasilisha utetezi wao kwa Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi Tanzania kutokana na utendaji wao kutoridhisha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi hiyo, Godfrey Mbanyi, aliyasema hayo jana alipokuwa akitangaza matokeo ya watahiniwa wa mitihani yao ya bodi hiyo.

Alisema bodi hiyo imechukua hatua ya kuwaandikia barua maofisa hao ili kutoa utetezi wao kutokana na malalamiko kutoka kwenye taasisi wanazozitumikia kuhusu utendaji wao mbovu ambao umezisababishia hasara ambayo hakuweka wazi.

Aidha, alisema kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi 2021 bodi imetoa adhabu au kuwaondoa katika vitengo maofisa hao huku 21 wakihamishwa kutokana na makosa mbalimbali ya kuisababishia serikali.

Kuhusu matokeo ya mitihani ya bodi, mkurugenzi huyo alisema watahiniwa 1,216 walisajiliwa kufanya mitihani na kati yao 1,135 sawa na asilimia 93.3, walifanya mitihani hiyo.

Alisema kati ya watahiniwa hao waliofanya mitihani hiyo 683 walikuwa wanarudia mitihani hiyo huku 452 ni watahiniwa wapya.

"Watahiniwa 613 wamefaulu mitihani na 474 watarudia mitihani ya baadhi ya masomo huku 48 wakifeli masomo yote," alisema.

Pia alisema bodi itaanza kutumia mitaala mipya Novemba, mwaka huu, hivyo kuanzia sasa vituo na vyuo vinavyofundisha masomo yanayohusu fani hiyo, vianze kuwaandaa wanafunzi.



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda (kulia), akiongozana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angela Kairuki (katikati) pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, wakati wakiingia ukumbini kuhudhuria mkutano wa kuelezea mafanikio ya mkoa huo na serikali ya awamu ya sita jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Azimio usalama kazini lafika bungeni

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amewasilisha azimio la kujumuisha suala la usalama na afya mahali pa kazi lililopitishwa na nchi wanachama wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Azimio hilo lilipitishwa katika Mkutano Mkuu wa 110 wa ILO uliofanyika Geneva mwaka 2022 ambapo waziri huyo alihudhuria akiwa ameambatana na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Khadija Mwenda, pamoja na watendaji wengine wa ofisi hiyo.

Akiwasilisha azimio hilo mbele ya kamati hiyo, Waziri Ndalichako alisema ameona ni muhimu kuishirikisha kamati kuhusu azimio hilo ili kuishauri Ofisi ya Waziri Mkuu na OSHA ipasavyo kwenye suala la usalama na afya nchini.

"Waheshimiwa wabunge tumeona ni vyema tukawasilisha kwenu azimio hili ambalo limepitishwa na nchi wanachama wa ILO na nchi yetu ikiwamo. Kutokana na azimio hili, masuala ya usalama na afya mahala pa kazi yanakuwa si wajibu wa kisheria pekee bali haki ya msingi mahali pa kazi," alisema.

Alitaja misingi ya awali ya ILO ya haki mahali pa kazi ni pamoja na uhuru wa kujumuika na utambuzi wa haki ya majadiliano ya pamoja, kukomesha mifumo yote ya kazi za kushurutishwa na kulazimishwa, kukomesha ajira za watoto na kukomesha kwa ubaguzi kwenye ajira na mahali pa kazi.

"Kwa mujibu wa azimio hilo lililopitishwa mwaka jana, suala la usalama na afya mahali pa kazi unakuwa ni msingi wa tano wa haki katika maeneo ya kazi,"alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Joseph Mhagama, alimshukuru Waziri Ndalichako kwa jitihada anazofanya katika kuhakikisha kwamba kamati hiyo inawezeshwa kutekeleza jukumu lake la kuisimamia ofisi hiyo.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Mwenda, aliishukuru kamati kwa miongozo na ushauri ambao imekuwa ikiitoa katika kuendelea kuboresha masuala ya usalama na afya mahali pa kazi ambapo ameahidi taasisi yake kuendelea kufanya kazi kwa bidii pamoja na kutekeleza maelekezo na kufanyia kazi ushauri ambao umekuwa ukitolewa na Kamati hiyo.





## AJIRA MPYA POLISI

# 50,000 wajitosa nafasi 500, kamishna ataja sifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, amesema jeshi hilo linahitaji watu sahihi wa kutekeleza sheria na ndiyo maana linahitaji kuajiri watu hao ili kutoa huduma bora za polisi.

Kamishna huyo alitoa kauli hiyo jana makao makuu ya jeshi hilo, Kilimani visiwani hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu ajira mpya za polisi.

Alisema taaluma ya polisi katika sheria imebadilika, hivyo wanahitaji watu wenye viwango vya elimu vinavyoendelezwa ili kuwawezesha kukabiliana na hali ya sasa katika utekelezaji wa sheria.

"Tunapodhamiria kujenga Jeshi la Polisi lenye weledi, elimu ni muhimu sana na ikiwa tunataka kufaulu kwenye taaluma ya polisi, hatuwezi kukwepa jukumu la kuhakikisha tunaajiri watu wenye sifa mpya, uchumi, siasa na uhusiano wa jamii," alifafanua.

Kamishna huyo alisema kuna mambo mengi yanayoathiri taaluma ya polisi, hivyo kupitia ajira, wana jukumu la kuandaa watu watakaokuwa viongozi wazuri wa Jeshi la Polisi baadaye.

Alisema kuna malalamiko mengi yanayohusu utendaji usiokidhi matarajio ya watu na usiozingatia weledi, akisisitiza kuwa yametolewa na watu mbalimbali akiwamo Rais huku mitandao ya kijamii nayo ikiwa sehemu ya majukwaa yanayowalaumu polisi.

Alisema asili ya utendaji usioridhisha na usiozingatia weledi inaanzia kwenye kuajiri askari wapya kwa sababu kuajiri watu wasio na sifa kielimu ni kuendeleza tatizo.

Alisema jeshi hilo visiwani Zanzibar lina idadi kubwa ya askari wenye viwango vya chini vya elimu ambao hawaendelezeki kutokana na kukosa sifa na wale wachache wenye sifa za kujiendeleza hawataki kujiendeleza kitaaluma. "Polisi Zanzibar ina chuo kinachoendesha kozi ya Polisi Sayansi ili kuwajengea uwezo askari lakini cha kusikitisha, hakuna askari polisi Mzanzibari hata mmoja anayesomea kozi hiyo licha ya kuwa hakuna gharama yoyote wanayotozwa," alifafanua.

Kamishna huyo alisema athari za kushindwa kujiendeleza au kukosa sifa za kuendelezwa ni pamoja na askari kubaki na kiwango cha chini cha utekelezaji wa kazi za polisi na kukosekana maarifa yayohitajika kutekeleza kazi za polisi.

Alitaja athari zingine ni kushindwa kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya teknolojia na matumizi yake katika kutenda makosa ya jinai, hofu ya mabadiliko, malalamiko yanayohusu maslahi, kuchelewa kupandа cheo na kukosa fursa mbalimbali. Alisema wanalazimika kuajiri askari polisi watakaofunzwa na kufahamu vyema kukabiliana na hali ya sasa na kutumia teknolojia mpya kwa ufanisi ili kuimarisha usalamma wa raia na mali zao.

Alisema serikali inafanya kazi kubwa ya kuwavutia wawekezaji na watalii, hivyo kuna malalamiko mengi kutoka kwa wageni kutopokewa vizuri vituo vya polisi na malalamiko hayo hayajengi taswira nzuri ya nchi hasa kwa uwekezaji na utalii.

Alisema jeshi hilo lina uhitaji mkubwa wa askari polisi hasa katika taaluma mbalimbali ikiwamo afya, sayansi, teknolojia ya habari na mawasiliano na katika ajira mpya ambazo mchakato wake unaendelea, wanatarajia kuajiri vijana wasiozidi 500 wenye sifa na waliojitokeza ni zaidi ya 50,000 na wenye sifa ni zaidi ya 2,000.



Baadhi ya waandishi wa habari Zanzibar, wakijipongeza baada ya kumaliza mkutano wa kujadili masuala ya sheria mbalimbali zinazohusiana na taaluma yao, ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tuhuma za rushwa 230 zapokewa ZAECA

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) katika kipindi cha miezi minne kuanzia Septemba hadi Desemba mwaka jana, imepokea tuhuma 238 zinazohusiana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Ali Abdallah Ali, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake visiwani hapa wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema kati ya tuhuma hizo, 168 zinaendelea na uchunguzi, sita zimehamishiwa taasisi zingine kwa kuendelea na hatua ikiwamo Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji, tuhuma 19 zimefanyiwa udhibiti wa kutoa elimu na tuhuma 45 zimetolewa ushauri wa kisheria.

Alisema majalada 18 yamefikishwa kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria ikiwamo kuwafikisha mahakamani watuhumiwa.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo alisema kuwa kati ya tuhuma hizo 238, hakuna tuhuma zinazohusiana na rushwa ya ngono na bado kuna changamoto katika kuripoti aina hiyo ya rushwa.

"Kutoripotiwa kwa tuhuma za vitendo vya rushwa ya ngono haina maana kama vitendo hivyo havipo katika jamii, yawezekana vipo lakini bado kuna usiri katika kuripoti," alihadharisha.

Aliitaka jamii kutokuwa na muhali wa kuripori matukio hayo ambayo hayakubaliki kisheria.

Mkurugenzi huyo pia alisema ZAECA imeokoa Sh. 3,580,593,549 (bilioni 3.58) zilizolipwa kama madeni katika taasisi mbalimbali za serikali. Alisema Sh. milioni 194.83 zimerudishwa kwa wananchi kufuatia madai yao mbalimbali yaliyowasilishwa ZAECA na kufanyiwa kazi yakiwamo madai ya wafanyakazi 700 wa hoteli za kampuni ya Pilipili.

Alisema mamlaka hiyo imejikita zaidi katika kudhibiti vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi katika hatua za awali kwa lengo la kusaidia juhudi za maendeleo zinazofanywa na serikali.

Alisema mamlaka inafuatilia fedha za serikali zinazoingizwa kwenye miradi ya maendeleo na zinazotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya taasisi kwa lengo la kuzuia matumizi mabaya ya fedha hizo. "Pia tunaendelea kufuatilia miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za UVIKO-19 pamoja na miradi mingine ya serikali na kuzifuatilia taasisi za serikali na mashirika yenye makusanyo na matumizi makubwa ya fedha ili kubaini mianya ya upotevu wa fedha na ukiukwaji wa taratibu za kisheria," alisema mkurugenzi huyo.

# Vijana wanaotoka kaya maskini wapewa mafunzo

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MFUKO wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) kupitia Mpango wa Ufadhili kwa Vijana kutoka Kaya Maskini na Wanaoishi katika Mazingira Magumu, umewanufaisha takribani vijana 600 wa visiwa vya Unguja na Pemba.

Akizungumza jana na wataalamu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Mwalimu Suleiman Zahoro kutoka Chuo cha Mafunzo ya Amali DAYA - Pemba, alisema, mafunzo hayo ya ujuzi ni ukombozi kwa vijana wengi kutoka kaya maskini na walio katika mazingira magumu kwa kuwa yatawasaidia kujikwamua kiuchumi.

Zahoro alisema anafundisha umeme wa magari na anafarijika jinsi vijana wanavyojitoa na kujituma ili kupata ujuzi huo licha ya mazingira waliyotoka kuwa magumu kulinganisha na fani wanayosoma.

"Vijana hawa wana bidii sana na shauku ya kutaka kujifunza pamoja na ukweli kwamba wengi wao hawajui chochote kuhusu umeme wa magari ila bidii yao inatia moyo," alisema mwalimu huyo.

Mussa Muhamed Juma, mmoja wa vijana hao ambao wako kwenye mafunzo kwa vitendo, aliishukuru serikali kwa kuwakumbuka vijana wanaoishi kwenye mazingira magumu na kuwapatia mafunzo ya ujuzi bila malipo, akibainisha kuwa waliyatamani lakini hawakuwa na uwezo wa kuyagharamia.

Jumla ya vijana 600 wamenufaika na mafunzo hayo ya visiwani Unguja na Pemba kupitia mpango huo unaosimamiwa na TEA.

TEA ilipewa jukumu la kusimamia na kutekeleza mpango huo na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuwafikia vijana kutoka makundi maalum na wanaoishi kwenye mazingira magumu walio katika kaya zilizosajiliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ili wafaidike na mpango huo kwa kupatiwa ujuzi utakaowawezesha kujikwamua kiuchumi.



SHILOL
Uk.13



# KAKIUKA TALAKA?

ALIYEKUWA mke wa Haji Manara, Rushaynah ambaye hivi karibuni amekuwa gumzo kutokana na namna alivyoondoka katika ndoa yake, amezidisha joto baada ya kuonekana kuwa karibu na mwanamuziki nyota Harmonize.

Siku chache baada ya kupewa talaka na Haji Manara, mrembo huyo ameanza kujirusha katika picha mbalimbali akiwa na harmonize, jambo ambalo limeibua minong'ono kwamba wawili hao wapo katika pezi jipya.

Kuwa karibu kwa wawili hao, baadhi ya watu wameonekana kushangazwa baadhi ya watu, ambao wanaeleza Rushaynah ameharakisha kuanzisha uhusiano mpya na hivyo kuonekana kama amekiuka masharti ya talaka.

Watu waliokuwa wakitoa maoni yao kutokana na video za mrembo huyo ambaye alionekana akicheza mpira nyumbani kwa Harmonize na ile akifanya mazoezi akiwa na mwanamuziki huyo.

"Rushayna ameharakisha kuanzisha uhusiano mpya kwani hajamaliza masharti ya talaka ambayo inamtaka kukaa eda kwa muda wa miezi mitatu kabla ya kuamua kwenda kwa mwanaume mwingine," amesema Kasim Ungando.

Amesema kinachoonekana ni kama Rushaynah na Harmonize wanafafanua mchezo huo kama njia ya kuongeza umaarufu wao na si kulingana na sheria ya talaka kwa Waislam inavyotaka.

Hata hivyo, wengine walimpongeza kwa hatua hiyo, wakieleza hakuna sababu ya kujifungia ikiwa mtu hana matumaini ya kurudi tena.

BASI SAWA

# Jonathan Budju kutikisa Uganda



MWIMBAJI wa nyimbo za injili anayetamba nchini Canada, Jonathan Budju, amesema miongoni mwa mambo makubwa atakayoyafanya mwaka huu ni lile tamasha lake la kwanza jijini Kampala, Uganda.

Akizungumza na BT, Budju a.k.a Son of God, amesema hilo ni tamasha lake la kwanza barani Afrika na anatarajia kulifanya kwa ukubwa kwa sababu ana mashabiki wengi pande hizi.

"Nimefurahi kuweka wazi mpango wangu mwaka huu ni kukutana na mashabiki zangu pale Kampala, Uganda. Kule nina mashabiki wengi na nina amini watafurahi kuhudumiwa na mimi, bado sijatoa tarehe lakini ni hivi karibuni onyesho hilo litafanyika," amesema Jonathan anayetamba na wimbo Hosanna.

# Town Classic Band yaja na bonanza



BENDI mpya ya muziki wa dansi ya Town Classic Band, inatarajia kuanza bonanza mwishoni mwa mwezi huu.

Meneja wa bendi hiyo, Andrew Sekidia, alisema bananza hilo litakuwa linafanyika kila Jumapili, katika ukumbi wa Msasani Club, Kawe Dar es Salaam.

"Miaka mingi Msasani Beach Club hakuna burudani ya muziki wa dansi, hivyo tunataka kurejesha bonanza, ili mashabiki waburudike," alisema Sekidia.

Alifafanua kuwa bendi hiyo imedhamiria kurejesha hadhi ya muziki wa dansi na kwamba mojawapo ya kurejesha hadhi hiyo ni kuanzisha bonanza.



# Shilole amshukuru Makalla kumshika mkono

MWANAMUZIKI na mjasiriamali, Shilole, amemshukuru Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam, Amos Makalla, kwa kumsaidia kupata eneo jipya la kufanyia biashara yake ya chakula.

Shilole ambaye anamiliki migahawa ya Shishi Food, alipatwa na tukio la kutakiwa kubomoa mgahawa wake baada ya eneo hilo kupangwa kujengwa kituo cha afya.

"Namshukuru Mkuu wa Mkoa, Amos Makalla na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe kwa kunipatia eneo lingine na sasa naanza kulijenga upya ili wateja wangu wapate huduma," amesema Shilole.





# 'Hirizi Mzigo' yamwibua Isha Mashauzi

MWANAMUZIKI nyota wa taarabu nchini, Isha Mashauzi, ametoa singo yake mpya 'Hirizi Mzigo' akisema ni mwanzo mpya wa kuurejesha muziki huo katika soko.

Akizungumza na BT, Isha Mashauzi, amesema ngoma hiyo ni mfululizo wa kazi anazotarajia kuzitoa 2023 ambazo zitaleta mwamko kwa mashabiki ambao wamerudi nyuma kutokana na kudorora kwa muziki huo.

"Huu ni mwanzo mpya wa kuirejesha taarabu katika kiwango chake, Hirizi Mzigo umeanza kuleta amsha amsha kwa mashabiki kiasi ambacho napata matumaini ya kurudi kama zamani," amesema Mashauzi.

# Michepuko kumbe tangu 'longi'

**Na Adam Fungamwango**

INADAIWA kwa miaka ya sasa kuna ongezeko kubwa la usaliti kwenye mapenzi au ndoa, kwani tunashuhudia idadi kubwa ya wapenzi au wanandoa wakiachana kwa sababu hiyo.

Wanaume wamekuwa wakitoka na wanawake wengine wakiwa ndani ya ndoa, wakiwa na wachumba au wapenzi wao. Wanawake pia nao wamekuwa wepesi kuchepuka na kutoka nje ya ndoa, au hata ana mchumba anayetaka kumuona au mpenzi wake wa kudumu, bado anakuwa na mwingine wa pembeni.

Hii imesababisha wengi kuchukia ndoa, au kutaka kuwa peke yao bila mpenzi.

Hata hivyo, imebainika kuwa jambo hili liko tangu zamani, enzi na enzi za mababu zetu.

Kinachotakiwa siyo kuacha kuoa au kuolewa, ila ni watu kuishi kwa hofu ya Mungu, kufanya sala na kumuomba aepushe mabaya yote.

Ukitaka kuthibitisha hili, hebu angalia nyimbo hizi za zamani ndiyo utajua kuwa kinachowapata watu leo hii, kiliwapata wengine huko nyuma.

**Edita-DDC Mlimani Park**

Edita ni wimbo uliopigwa na bendi ya DDC Mlimani Park. Maudhui yake ni kwamba jamaa anamtimua mpenzi wake baada ya kumfumania nyumbani kwake akiwa na mwanaume mwingine.

Anamwambia kuwa aliambiwa na majirani siku nyingi kuhusu tabia yake, lakini alidhani ni fitina tu, lakini leo ameamini kwani amemfuma laivu.

Anamwambia ndiyo maana kila akirejea nyumbani hamkuti na akirudi anamwambia alikuwa kwa shangazi Kariakoo, kumbe anakwenda kwa bwana 'ake. Lakini haikutosha, sasa ameamua amlete hadi nyumbani hapo wanapoishi. Mwisho anamwambia achukue kila chake aondoke.

**Milima ya Kwetu-Super Rainbow**

Wimbo huu ulitungwa na marehemu Eddy Sheggy, akiwa na Super Rainbow. Mtunzi anarejea kwao Lushoto, akiwa anaitazama milima ya kwao. Akiwa ndani ya basi anakumbuka siku alipotoka kwao Lushoto kwenda Dar alikuwa na mkewe, lakini sasa anarejea peke yake. Atakwenda kuwaambia nini wazazi, ndugu na marafiki? Nini kilitokea wakiwa Dar.

Ni kwamba baada ya kufika Dar, mkewe akachangamka. Akawa anajua zaidi kuliko mumewe. Akawa mtoto wa mjini. Kila bwana wa kwake. Akaanza kumfanyia visa mumewe. Hali ikawa mbaya mpaka mwanamke akatoroka na kumuacha mumewe akiwa hana la kufanya.

**Baba Jenny-Hamza Kalala**

Hamza Kalala alitunga wimbo wa 'Baba Jenny', akisimama kama mwanamama anayelalamika kuhusu visa vya mumewe.

Mama huyo anadai kuwa gari la mumewe hajawahi kupanda hasa siku moja, zaidi ya kulijua kwa honi, kukosha na kufuta vumbi, pamoja na muungurumo.

Gari hilo linatumika zaidi kumbeba kimada wa mumewe na kwenda naye kwenye starehe.

Mbaya zaidi ni siku moja mumewe alipompita kwenye kituo cha basi akiwa na watoto mvua kubwa inanyesha, lakini jamaa ndani ya gari alikuwa na kimada wake akawapita kama hawajui.

Mwisho anamuaga mumewe bai bai, yamemfika shingoni, anaondoa, siyo kama hampenzi, lakini tabu zimezidi.

**Stendi ya Basi-Orchestra Tomatoma**

Ukitaka kujua kuwa watu walikuwa na wasiwasi wa wake au waume zao kuchepuka sikiliza kisa hiki kwenye wimbo wa 'Stand ya Basi'.

Hapa mume anamuuliza mkewe kuwa kila siku anarudi usiku kutoka kazini, halafu hakuelewielewi, sababu ni nini hasa?

Mke anamjibu kuwa anachelewa stendi ya basi, kwani kuna tabu sana ya mabasi na hakuna asiyejua hilo.

Ikumbukwe kuwa miaka ya '80 hadi mwanzoni mwa '90 Dar ilikuwa na tatizo la usafiri, lakini kwa sasa kama kweli huyo dada anachelewa kwa mchepuko, angeweza kumdanganya mumewe kuwa anachelewa kwa sababu ya foleni.

**Baba Shaaban-Juwata Jazz band**

Ulikuwa ni utunzi wa marehemu Shaaban Mbwembwe, ukimzungumzia mwanamama mmoja akimuuliza mumewe anasikia kwa majirani kuwa ana mchepuko huko nje anayempenda sana.

Mumewe anamjibu kuwa asiwasikilize kwa sababu nia yao wanataka watengane ili wawacheke na hizo zote ni fitina za maisha yao mazuri kuliko ya kwao.





# Wagunda Empire: Ufalme wa mchongo

**Na Adam Fungamwango**

KILA mtu anajua amefika kwenye kilele chake cha mafanikio kwa njia gani. Wengine wamefika kwa juhudi zao. Wengine wamepandishwa kwa msaada wa watu wengine. Lakini wapo waliofika hapo kwa ujanja ujanja, wakati mwingine kutoa kafara na ushirikina.

Halafu watu waliopata mafanikio kwa njia zisizo halali mara nyingi wanakuwa na kiburi na kutesa wenzao, husuan wale wa chini yake.

Kwenye dunia hii tumeshaona mengi na tumeona watu wengi ambao baada ya kupata ukubwa, madaraka, cheo au mali, wanabadilika kabisa. Sasa ukute ndiyo kapata kwa sababu anazozijua mwenyewe.

Jacob Mweche ameandika filamu iitwayo 'Wagunda Empire'. Inashabihiana kabisa na hiki ninachokisema, walioshiriki ni Jacob Mkweche, Amani Solomon, Juma Kibwana, Martin Manyiri, Rehema Daniel na wengineo.

Mfalme wa himaya moja ya Wagunda, ana kijana wake ambao anataka kumrithisha ufalme. Lakini kabla hapo awe ameoa. Mfalme anaita warembo wote wa kijiji hicho ili achague mmoja wapo. Hakuna aliyempenda. Mfalme anafadhaika. Siku moja akiwa matembezini na walinzi wake wanamuona msichana mmoja ambaye ghafla tu, mwanamfalme anatokea kumpenda.

Aliporudi nyumbani aliwatuma walinzi wamfuatilie, huku akimwambia baba yake tayari amempata msichana anayempenda.

Walinzi walimkuta msichana yule akiwa na mpenzi wake kwenye himaya nyingine.

Mfalme anatuma watu kwenda kumuua mpenzi wake na kumleta msichana huyo. Msichana alisema wazi kuwa analazimishwa, lakini hampendi mtoto wa mfalme. Wananchi wa himaya nyingine wanachachamaa. Wanatumwa watu wawili kwenda kuongea na mfalme ili awarudishie mwananchi wao. Mfalme anapomuona mmoja wa mtu aliyekuja hapo ananywea na kumuamuru kijana wake kumuachia mara moja msichana huyo.

Mtoto wa mfalme alionekana kupinga, lakini baba yake alikuwa mkali kitu ambacho alikuwa hajawahi kukiona.

Alishangaa kwani alijua kwa jinsi anavyomfahamu baba yake kwa wale watu wawili tu, angeweza kuwakamata na kuwanyonga.

Msichana huyo alikuwa tayari mjamzito na alipofika kwenye himaya yao wakamuuliza kama ujauzito ule ni wa mwanamfalme alipinga na kusema ulikuwa na wa mchumba wake waliyeuawa na mfalme.

Akasema alipelekwa kwa mwanamfalme akiwa tayari mjamzito, lakini aliogopa kusema.

Bwana Ndevutatu akaanza kutoa siri kuwa ni kwa nini mfalme alipomuona alikubali kuwakabishi msichana haraka. Akasema zile ndevutatu alizokuwa nazo ni uhai ya mfalme yule, mkewe na mtoto wao. Akafichua kuwa miaka mingi nyuma, alitaka uwe mfalme badala ya ndugu zake. Mganga akamwambia atafute mwanamke mjamzito, halafu akijifungua, mama auawe na mtoto awe ndiyo kafara.



# Pole sana Mercy

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Mercy Johnson Okojie, amefunguka kuhusu vita yake anavyopitia dhidi ya ugonjwa wa saratani na upasuaji aliofanyiwa.

Johnson akizungumza katika kipindi chake kinachoitwa, 'Mercy's Menu,' akiwa na Joke Silva, amesema tabu zote amekuwa akisaidiwa na

mumewe, Olu Jacobs.

Amefichua kwamba yeye na mumewe walipaswa kukabiliana na ukweli wao mpya na kila kitu kilianza ukurasa mpya.

Amesema aligundua tatizo hilo wakati mtoto wake wa mwisho akiwa na umri wa miezi 6 na wakati wa upasuaji, aligundua kuwa alilazimika kuishi kwa kutumia dawa maisha yake yote.



## Kanye West imekuaje ukaoa kimya kimya?

RAPA maarufu wa Marekani, Kanye West, ameripotiwa kufunga ndoa ya siri na mbunifu wa mavazi ya Yeezy anayeitwa Bianca Censori.

Inaelezwa ndoa hiyo ilifungwa miezi miwili baada ya kukamilika zoezi la kupeana talaka na aliyekuwa mkewe Kim Kardashian.

Mapema wiki hii, mwanamuziki huyo aliibua mjadala baada ya kuonekana na Censori, ambaye anajulikana kama mwanamke mwenye mambo mengi.

Hata hivyo, taarifa zilizotoka hivi karibuni zinasema wawili hao wamefunga ndoa ya faragha.

## Bank hata iweje mtakwenda mafunzo

MWIMBAJI wa muziki na mwanasiasa maarufu, Olubankole Wellington, maarufu Banky W, amesema mafunzo ya kikosi cha Huduma ya Vijana kwa Kitaifa (NYSC), hayapaswi kuwa ya lazima, bali hiari ya mtu.

Mwanamuziki huyo alitoa maoni yake katika mahojiano na televisheni, akisema kuwa mpango wa NYSC haujafikia lengo la uundwaji wake.

"Sijui kama kuna mtu ambaye atapingana na mimi kwamba NYSC labda haifanikiwi lengo la kuundwa kwake, kwa hivyo tunairekebishaje? Amehoji.





## Itanoga hapa Wizkid pale Davido

MASHABIKI wa muziki nchini Nigeria, wanatarajia kufanya tamasha la kipekee baada ya nyota wawili wanaopendwa zaidi nchini humo, Davido na Wizkid wakitumbuiza kwenye jukwaa moja.

Wizkid ametumia ukurasa wake wa Instagram na kuweka tangazo lililowashangaza wengi kuwa atafanya maonesho ya muziki na nyota mwenzake wa muziki, Davido.

"Baada ya ziara yake ya 'MLLE (More Love, Less Ego)' Mimi na Davido tutafanya maonesho kwa pamoja! Ili kuokoa pesa yako," ameandika Wizikid.

Inakumbukwa kuwa Wizkid aliripotiwa kuahirisha kutoa albamu yake ya tano ya 'More Love, Less Ego' kufuatia kifo cha mtoto wa Davido, Ifeanyi.

## Ka3na usiwataje yaweza kuwa...

ALIYEKUWA mshiriki wa shindano la Big Brother Nigeria, Ka3na ametishia kuwafichua wanaume wote wenye ndoa ambao wanamsumbua kwenye DM yake wakimtaka kimapenzi.

Nyota huyo alibainisha kuwa wanaume hao walifanya mazungumzo naye vyema na kwamba wanamuhatarishia kumwambukiza virusi siku zijazo.

"Saa 24 zijazo nitawaanika wanaume wote waliooa kwenye DM yangu. Inatosha. Inatosha. Unathubutuje kuwa na familia nzuri kwenye ukurasa wako na ukawa bize kufanya kazi za shetani kwenye DM yangu? Amehoji.



## DC aweka mtegoni watendaji wa vijiji

**Na Oscar Assenga,** PANGANI

MKUU wa Wilaya ya Pangani, Ghalib Ringo, amewaweka 'mtegoni' maofisa watendaji wa vijiji, kwa kuwalinda wenyeviti wao kutokutoa taarifa za mapato na matumizi kama kanuni inavyoelekeza.

Viongozi hao wanatakiwa kubandika taarifa za mapato na matumizi ili kuwaondolea sintofahamu wananchi juu ya matumizi ya fedha zinazotolewa kwa ajili ya miradi na maendeleo ya vijiji.

Aidha, alisema tabia ya kusomwa kwa taarifa hizo kwa wananchi kila kipindi cha robo ya mwaka, inasababisha migogoro ambayo huwafanya wananchi wakati mwingine kugoma kushiriki shughuli za maendeleo, kama kuchangia miradi mbalimbali kwa kuhofia fedha zao kutafunwa.

Kauli hiyo ya Ringo, inaunga mkono kauli iliyotolewa hivi karibuni na Goodluck Malilo kutoka Asasi ya Kijamii ya Tree of Hope, ambaye ni mratibu wa mradi wa uhamasishaji wa jamii na mamlaka husika wa kuboresha elimu, alisema tatizo kubwa linaloitesa jamii kwa sasa ni kutokubandikwa kwa taarifa za mapato na matumizi kwenye mbao za matangazo kwenye ofisi za vijiji.

"Bila elimu hatuwezi kufika kokote, lakini lazima viongozi wa vijiji na kata waone umuhimu wa kuwajibika, kwa kuhakikisha kuna kuwapo na uwazi katika mapato na matumizi ya fedha za umma.

"Hata hivyo, nasikitishwa sana na wadau na wasimamizi wa elimu kutokuhudhuria kwenye vikao hivi, ambavyo ni muhimu kwa ustawi wa maendeleo ya elimu. Nilichokiona ni kukosekana kwa utawala bora na uwazi katika ngazi ya vijiji, kwa sababu ni dhahiri kwamba ukiweka taarifa ya mapato na matumizi kwenye mbao za matangazo, unatengeneza uwazi.

Zaidi aliongeza, "Sasa inakuwaje watendaji wa vijiji na mabosi wao wa kata, wanakaa kimya mwaka mzima bila kusoma mapato na matumizi? Na hiki ndio kigezo cha utawala bora," alisema.

Tree of Hope inatekeleza mradi huo wa uhamasishaji unaolenga kuinua kiwango cha elimu katika kata nne za Wilaya ya Pangani, kwa ufadhili wa Shirika la The Foundation For Civil Society (FCS).

Awali, Malilo alinukuliwa akisema miongoni mwa matatizo yaliyojitokeza kwenye robo ya kwanza ya mradi huo ni viongozi wa vitongoji, kutokuitisha mikutano ya kikatiba ya kila mwezi, hivyo wananchi kukosa fursa ya kukusanyika na kujadili maendeleo yao, hususani yale yanayohusu elimu.

Alisema kukosekana kwa vikao hivyo, kunasababisha wananchi kushindwa kuelewa miradi inayoendelea katika maeneo yao na kujikuta wakiwalaumu viongozi kutokana na kushindwa kutimiza wajibu wao wa kikatiba.

# Wakamatwa madai kuficha watoto kujiunga na masomo

**Na Hamida Kamchalla,** HANDENI

WATU sita wamekamatwa kwa amri ya Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Siriel Mchembe, kwa tuhuma za kuficha taarifa za watoto wao kukatisha masomo shuleni kutokana na kupata ujauzito.

Kamata kamata hiyo iliyoongozwa na Mchembe, pia imewahusisha wanafunzi ambao wameshindwa kuripoti shuleni kwa zaidi ya wiki moja tangu kufunguliwa kwa shule zote nchini Januari 9, mwaka huu.

Akizungumzia operesheni hiyo jana, Mchembe alisema wamewakamata wazazi na wanafunzi hao, lakini yuko mwanafunzi wa darasa la tano, ambaye aliolewa katika kipindi cha likizo.

"Ukitaka uwe salama katika wilaya hii ninayoiongoza, wazazi na walezi ni lazima wahakikishe kwamba watoto wao wanakwenda shule. Ukifanya hivi pia utaepuka faini ambazo zinatozwa kwa mtoto ambaye hajafika shuleni.

"Katika operesheni hii, tumewagundua watoto watatu ambao ni wajawazito, lakini yupo mwingine mmoja ambaye wazazi wake, hawataki binti yao aende shule. Vilevile katika Kijiji cha Kwamatuku, yupo msichana mmoja mwenye umri wa miaka 13 na yuko darasa la tano ameolewa," alisema. Aidha, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Handeni, Mussa Mkombati, akizungumzia makali ya operesheni hiyo, aliwasihi wananchi wa eneo hilo kutoa ushirikiano kwa serikali, kwa kuwafichua watoto walioshindwa kuripoti shuleni au wenye ujauzito.

"Kwa wananchi watakaosaidia kutoa taarifa kuhusu mambo haya, nitatoa zawadi ya fedha kwa atakayefichua siri hiyo, lakini atakayetoa taarifa tutamlinda na hatotajwa jina kwa wahusika," alisema Mkombati.

Kadhalika, Mwenyekiti wa CCM wa Kata ya Kwamagome, Salim Magulwa, aliwashauri viongozi wa chama hicho, kuacha tabia ya kujiingiza katika ukatili huo wa kuzuia watoto nyumbani, kwa kuwa atakayebainika atachukuliwa hatua za kisheria.

Mpaka sasa wanafunzi walioripoti shuleni katika Halmashauri ya Mji wa Handeni ni asilimia 42 na kwa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ni asilimia 62.



Meneja wa Shule ya Awali na Msingi Glisten ya Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Justice Nyari, akizungumza kwenye kikao kazi cha uboreshaji wa usimamizi wa elimu ya msingi na sekondari, mjini Babati mapema wiki hii. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wafanyakazi wamwangukia Waziri Ndalichako

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ZAIDI ya wafanyakazi 200 waliokuwa wafanyakazi wa hoteli ya Sabasaba, mkoani Arusha, wamemwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Kazi na Ajira, kuingilia kati suala la kutolipwa stahili zao za mishahara inayofikia Sh. milioni 200.

Akizungumzia madai hayo, mmoja wa wafanyakazi hao, Ramadhan Issa, alisema wafanyakazi 220 waliokuwa wakifanya kazi katika Hoteli ya Sabasaba, walisitishiwa ajira zao, Agosti 31, 2000.

Issa alisema tayari serikali ilifanya ufuatiliaji na uhakiki ili kubaini kila mfanyakazi alistahili kulipwa kiasi gani cha fedha na kazi hiyo ilifanyika vizuri, lakini hadi sasa hakuna majibu.

"Kazi ilifanyika vyema, lakini tatizo lilikuja kujitokeza kwa waliokuwa viongozi wa hoteli, kutotii maelekezo ya serikali katika mchakato wa ulipaji wa stahiki za wafanyakazi hao," alisema.

Hata hivyo, alisema uongozi wa hoteli hiyo, haukufuata mwongozo na maelekezo ya serikali ya kulipa wafanyakazi stahiki zao badala yake ulitengeneza uongozi mwingine tofauti na ule uliokuwapo na kuwalipa fedha ambao siyo kama ilivyoelekezwa na serikali.

"Baada ya kugundua tatizo hilo tulilalamika kupitia iliyokuwa Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) na walituma mjumbe kuja kusikiliza madai yetu na tulifanya kikao na kuwaeleza kuwa wakati wa malipo tulipunjwa fedha na waliagiza uongozi kutengeneza tena taarifa ya pili ambayo itajazia mapunjo ya fedha yaliyotokana na yale ya mwanzo,"alisema.

Alisema malipo ya awali yalikuwa Sh. milioni 217, lakini fedha hizo zilichakachuliwa na uongozi na baada ya malipo ya awamu ya pili wafanyakazi 1,014 walitolewa nje ya hoteli kwa kupunguzwa na walibakia wafanyakazi 106 kwa ajili ya kulinda hoteli wakisubiri mwekezaji.

"Baada ya hizo fedha kutolewa sisi tulikuwa nje na meneja alizipokea Januari 11, 2001 tulitarajia tungeitwa ili kulipwa fedha zetu kwa kuwa aliagizwa fedha zitakapotolewa aitishe kikao kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi kwa kuwa kila mtu alitakiwa kufahamu analipswa kiasi gani kwa awamu ya pili," aliongeza.

Aliongeza kuwa meneja huyo aliandika barua serikalini kuwajulisha kwamba amekamilisha shughuli ya kuwalipa stahiki zao na hawadai kitu chochote ilhali Sh. milioni 273.8 hawakupewa alidai zilichukuliwa na kiongozi huyo.

Naye Janeth Elienea, alisema wanaishukuru serikali kwa kuwatendea haki kwa kutoa fedha hizo, lakini hapakuwapo kwa usimamizi mzuri wakati wa ugawaji ili kufanikisha kupata stahiki zao na ofisi za serikali za ngazi zote zinafahamu madai hayo.

"Tunajanga kubwa watoto hawaendi shule, tuna watu wanatutegemea wakiwamo wazazi ambao kwa sasa ni wazee na wanahitaji msaada hivyo tunaiomba serikali itilie mkazo jambo hili, kwa kuwa tumedai kwa muda mrefu," alisema.

TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOKWENDA

# Wasukaukili, washona mikeka wanavyotoweka kimya kimya

Na Adam Fungamwango



ZAMANI maeneo ya Pwani hasa sehemu za Dar es Salaam, Zanzibar, Bagamoyo, Lindi na Mtwara unapopita mitaani huwezi kumaliza mitaa minne bila kukutana na mama au msichana akiwa ameketi barazani anasuka ukili.

Miaka ya 1990 kurudi nyuma ilikuwa ni jambo la kawaida tu kukuta mama, msichana mmoja au wawili au zaidi wakiwa amekaa wanasuka ukili, huku wakipiga stori za kila siku zile za hapa na pale, huku watoto wao wakicheza pembeni.

Nakumbuka mama yangu naye alikuwa mmoja kati ya kinamama hao. Alikuwa akienda sokoni kununua ukindu.

Ukindu ni majani au kitembe ambayo hupatikana sehemu mbalimbali, hususan kwenye mito au zenye kupitiwa maji mara kwa mara. Majani yake hutumika kusukia kili za kushonea vikapu, mikeka au vitanga.

Baada ya hapo atarudi nyumbani na kuanza kuchana ukindu kwa namna ambayo anahitaji ili kusuka ukili.

Nilikuwa nikimwona mama yangu akisuka ukili karibuni kila siku anapopata nafasi. Mara nyingi huwa baada ya chakula cha mchana au jioni kabla ya kupika chakula cha jioni, ingawa kuna wakati pia alikuwa anapumzika kufanya kazi hiyo.

Hata majirani zake nao walikuwa wanafanya hivyo hivyo. Wakati mwingine wanakusanyika pamoja kupiga stori huku akisuka.

Nilichokuwa nakiona ni kwamba kila siku ukili ulikuwa unakuwa mrefu na kukunjwa mithili ya nyoka aliyejikunja.

Anaporidhika kwa mahesabu ya macho, nilichokuwa nikikiona alikuwa anapima kwa kutumia urefu wake na mkono kuunyoosha juu akiwa ameshika ukili. Atafanya hivyo mara kadhaa akihesabu hadi pale atakaporidhika au hesabu ya urefu anaoutaka utakapopatikana. Hadi mama yangu mzazi anafariki sijawahi hata siku moja kumuuliza huwa wanahesabu hivyo mara ngapi.

Tulichokuwa tunaona na kuburudika kuwaona pale tulipokuwa watoto ni kuona tu wanavyosuka na kushona tu, si kuuliza maswali.

Halafu sasa mama yangu alikuwa mmoja wa wale kinamama aliyekuwa akianza kusuka, anaimba anaimba. Ataimba nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania. Akichoka ataimba nyimbo za mapambio, akimaliza anaimba nyimbo za kiasili za nyumbani kwao alizaliwa.

Kwetu sisi ilikuwa ni burudani tu. Kwanza ile kumuona anasuka ukili ilikuwa tunapenda kumuona. Halafu kama dakika 10 zikipita tunamkumbusha, "mama leo mbona huimbi?"

Hajibu kitu, muda si mrefu ataanza kuimba. Sisi watoto wake tunakaa kimya kumsikiliza na kupata burudani ya nyimbo hadi atakapochoka kusuka, au muda wa kuanza kuandaa chakula.

Baada ya kupata mikanda kadhaa ya ukili ambayo nilisema ni kama nyoka aliyejikunja. Siku moja atakwenda sokoni kununua rangi mbalimbali ambazo kuna atazichemsha kwa kuchanganya maji. Baada ya hapo atatumbukiza ukili aliousuka kwenye maji yaliyochezwa na rangi. Kila ukili utakuwa utatumbukizwa kwenye maji ya rangi inayotakiwa. Mmoja utawekwa kwenye rangi nyekundu, mwingine bluu na mwingine kijani. Halafu kuna ukili mmoja au miwili haitawekwa popote. Utabaki na rangi yake ya asili.

Siku chache baadaye utaanza kuona mama anaanza kushona yale maburungutu ya mduara ya ukili wenye rangi tofauti.

Nilikuwa namuona mama yangu akishona kwa kutumia sindano kubwa na ndefu. Uzi aliokuwa akitumia mara nyingi ni wa nailoni.

Ushonaji huo nao utakuwa kwa muda wa zaidi ya wiki moja au zaidi kutegemea na kazi zake zingine. Halafu siku isiyo na jina unaona anataka kwa kisu mviringo wa mshono ule na kuwa mkeka. Na urefu au ukubwa wake unategemea na saizi aliyokuwa akiihitaji tangu awali.

Mkeka huo unakuwa na rangi mchanganyiko ambazo alikuwa wakichovya ukili wake kwenye yale maji yaliyocheshwa na kuchanyikana na rangi.

Kinamama wengine huuza mikeka huyo, mingine hutumika kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya familia yake na wageni tu nyumbani.

Huu ni usanii wa hali juu ambao kinamama wa wakati huo hasa wa maeneo ya Pwani, waliozaliwa, kukulia, au kuishi walikuwa nayo.

Anapoanza kusuka ukili unaweza kuona kama anajichosha au kupoteza muda, lakini mwisho wa siku hata sisi wenyewe watoto tulikuwa tunashangaa mwisho wa yote unaibuka mkeka.

Cha kusikitisha ni kwamba siku hizi unaweza kutembea na kuimaliza Dar es Salaam yote, tena siku hizi ni kubwa sana kuliko zamani na usimkute mama anasuka ukili au kushona mkeka.

Utamaduni au sanaa hii ambayo ilitakiwa kuendelezwa vizazi kwa vizazi imeanza kupotea kama si kupotea kabisa. Sidhani kama kinamama walikuwa wamewarithisha mabinti zao. Au kama walirithishwa wanaona umuhimu huo kwa sasa?

**Tuma meseji 0716 350534**



# Washirika wa Ukraine wajadili kutoa vifaru

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine, Volodmir Zelensky, amewataka washirika wake wa Magharibi kutoa msaada zaidi wa kijeshi ili kukabiliana na vikosi vya Russia.

Akizungumza jana kiongozi huyo ameionya Russia kutaka kujipa mamlaka ya kuharibu mataifa mengine, alisema lazima ishindwe.

Zelensky amewaambia wajumbe kwenye mkutano na mataifa zaidi ya 50 yanayojiandaa kuisaidia Ukraine kwa silaha, kuwa umakini unatakiwa katika suala la kutoa kuwapa vifaru vya kisasa.

Washirika wa Ukraine walikutana jana ili kuratibu usambazaji wa silaha kwa nchi hiyo ambayo kwa sasa imeongeza maombi yake ya kupewa vifaru vya kivita.

Ujerumani inakabiliwa na shinikizo kubwa kuruhusu vifaru vinavyosemekana kuwa vya ubora wa juu zaidi vya Leopard kusafirishwa kwenda Ukraine.

Mazungumzo hayo magumu yanafanyika siku moja baada ya Marekani na mataifa kadhaa ya Ulaya kuahidi vifaa zaidi vya kusaidia Ukraine kukabiliana na mashambulizi yoyote zaidi ya Russia.

Uingereza pia ilitoa vifaru 14 vya kivita hivi karibuni, lakini Ukraine inataka vifaru zaidi.

"Vifaru kwa Ukraine ni kwa ajili ya uhuru," Yuriy Sak alisema katika kipindi cha Newsnight cha BBC.

Zaidi ya mataifa 50 yanatarajiwa kukutana katika kambi ya anga ya Marekani ya Ramstein kusini-magharibi mwa Ujerumani.

Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz anakabiliwa na shinikizo kubwa la kuchangia vifaru viwili vya Leopard, kufuatia uchangiaji wa hivi majuzi wa Uingereza wa vifaru 14 ya kivita vya Challenger.

Kama taifa la utengenezaji silaha, Ujerumani lazima itoe idhini yake kabla ya nchi zingine kujitolea kutuma vifaru vyao wenyewe vya Leopard.

Waziri mkuu wa Poland alisema anakata tamaa kuhusu kupata baraka za Ujerumani, ingawa waziri wa Lithuania aliambia shirika la habari la AFP kwamba baadhi ya nchi zitatuma vifaru vya Leopard.

Ujerumani ilisema msimamo wake utakuwa wazi katika saa chache zijazo kuhusu suala hilo.

**BBC**



Wakazi wakiangalia masalia yaliyobaki katika fukwe ya Reo Del Mar, Calfonia nchini Marekani kutokana na kimbunga kupiga eneo hilo hivi karibuni na kuharibu makazi ya watu. **PICHA: AF**

# Rwanda yaelemewa na wakimbizi

**KIGALI,** RWANDA

RWANDA imetangaza kuweka kambi za dharura kwa wakimbizi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wanaoendelea kuingia nchini humo wakikimbia kile wanachosema kuwa mauaji dhidi ya wanaozungumza lugha ya Kinyarwanda.

Wakimbizi zaidi ya 1,200 wako katika kambi hizo kaskazini magharibi mwa Rwanda.

Hatua hiyo inafuatia siku chache tu baada ya Rais wa Rwanda, Paul Kagame, kutoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuwajibika katika suala la wakimbizi wanaotokana na mzozo wa mashariki mwa DRC.

Kambi ya Nkamira iliyoko wilaya ya Rubavu, ina wakimbizi zaidi ya 600 wakati kambi ya Kijote umbali wa kilomita sita kutoka eneo hilo ikihifadhi watu zaidi ya 500.

Waliozungumza na BBC kutoka kambi ya Nkamira, walisema mbali na vita kati ya kundi la M23 na serikali ya DRC na makundi mengine ya waasi, kuna mauaji dhidi ya Watutsi na uharibifu wa mali zao ikiwamo mifugo.

Mupenzi Nshizirungu alitoka eneo la Kagusa, alisema alilazimika kuacha ng'ombe wake baada ya baadhi kukamatwa na kuchinjwa kiholela.

"Walinikuta nikichunga ng'ombe wangu baada ya kuchinja baadhi ya ng'ombe wengine waliwaua kiholela nikaona heri kuacha ng'ombe na kulinda usalama wangu," alisema. Aliongeza kuwa wametimuliwa katika maeneo yao asilia 'kwa kuhusishwa na wapiganaji wa M23 wanaoipinga serikali.

Kituo cha afya kimeanzishwa katika kambi hiyo kuwasaidia wakimbizi walioko katika hali mbaya za kiafya na kwamba mashirika ya misaada yanatoa huduma kwa wakimbizi hao.: BBC

Kulingana na msemaji wa shirika la wakimbizi UNHCR, Lilly Carlisle, wakimbizi hao wanapata msaada wa dharura kabla ya uwezekano wa kuhamishwa katika kambi nyingine mbali na mpaka wa DRC walikotoka.

Baadhi ya wakimbizi walisema kambini kuna matatizo ya malazi na chakula kisichobadilika tangu walipofika "Wanalala kwenye mikeka na kula mahindi kila siku," lilisema shirika hilo.

Rwanda inahifadhi wakimbizi wa DRC zaidi ya 72,000 ambao waliotoroka vita na machafuko mashariki mwa nchi yao zaidi ya miongo miwili iliyopita.

Shirika la UNHCR lilisema kwamba mwishoni mwa mwezi Novemba, kuwa wakimbizi takriban 3,000 walikimbilia nchini Rwanda na kuhamishwa katika kambi ya Mahama mashariki mwa nchi hiyo.

Mapema mwezi huu Rais wa Rwanda, Paul Kagame, alisema nchi yake imechoka kwendelea kubebeshwa mzigo wa matatizo ya Congo.

Rwanda ilisema haina nia ya kuwafukuza au kuwapiga marufuku wakimbizi na kusisitiza, daima inakaribisha watu wanaokimbia ukosefu wa usalama, mateso na vurugu, lakini ikatoa wito kwa Jumuiya ya kimataifa kuchukua jukumu la kutafuta suluhu ya kudumu kwa kundi hilo la wakimbizi kutoka DRC ililotaja kuwa lilisahaulika.

Mvutano kati ya DRC na Rwanda umeendelea licha ya juhudi za kidiplomasia kutatua mzozo unaodaiwa kuunga mkono makundi hasimu.

**BBC**

## Vikosi vya Eritrea vyaondoka Tigra

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

WAKAZI kutoka maeneo tofauti ya jimbo la Tigray, wamethibitisha kuwa wanajeshi kutoka nchi jirani ya Eritrea wanaondoka kwa wingi kutoka katika maeneo ambayo wamekuwa wakidhibiti.

Mtu aliyeshuhudia katika mji wa Adwa, aliambia BBC kwamba magari ya jeshi la Eritrea yamekuwa yakipita katika mji huo tangu jana asubuhi.

"Askari wamekuwa wakisafiri kwa magari mengi," alisema. Akielezea idadi ya askari hao kuwa sawa na mchwa kwa wingi wao, pia magari hayo yalikuwa yakipiga tarumbeta na askari walikuwa wakiimba.

"Walikuwa wakiimba wakiwa na bendera kwenye magari yao," aliongeza.

Wakati huo huo, jeshi la shirikisho la Ethiopia lilikuwa likiendelea kulinda viunga vya mji, mkazi huyo alisema.

Kwa mujibu wa makubaliano ya amani kati ya serikali ya shirikisho na Chama cha Tigray People's Liberation Front (TPLF), uondoaji wa vikosi vya kigeni na vikundi visivyo vya shirikisho vyenye silaha kutoka Tigray ungefanyika wakati vikosi vya Tigray vitakabidhi silaha zao nzito kwa serikali ya shirikisho.

Mkazi mwingine wa mji wa Aksum, alisema aliona makumi ya magari yanayosafirisha wanajeshi wa Eritrea na silaha yakipita katika mji huo.

"Nimehesabu magari 70, vifaru 12 na vingine vingi. Wanajeshi walikuwa kwenye magari tofauti. Wanakuja upande wa Adwa na kuelekea mji wa Shire," Berihu Kahsay, ambaye alikuwa miongoni mwa wakazi waliokuwa wamejipanga barabarani kushuhudia kuondoka kwa askari hao.

Vyanzo kadhaa nchini Eritrea pia vimethibitisha kuondolewa kwa wingi kwa wanajeshi na zana za kijeshi. Wanajeshi wa Eritrea walipelekwa nchini humo Novemba 2020 kuunga mkono serikali ya Ethiopia dhidi ya wapiganaji wa TPLF huko Tigray.

**BBC**

# ACT yataka mazingira rafiki uwekezaji uzalishaji mbolea

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kutengeneza mazingira rafiki ili kuvutia wawekezaji zaidi kwenye uzalishaji wa mbolea nchini na kuviimarisha viwanda vilivyoko.

Pia kimeitaka serikali kubadili mfumo wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa kuiondoa kwa wasambazaji na badala yake iweke ruzuku hiyo kwenye mbolea inayoagizwa kutoka nje ya nchi.

Taarifa ya Waziri Kivuli wa Kilimo, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi wa ACT, Mtutura Mtutura, kwa vyombo vya habari jana ilieleza kuwa uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi utapunguza gharama za bidhaa hiyo, hivyo kuongeza uzalishaji.

Mtatura alisema ruzuku ikiwekwa kwa waagizaji wa nje itawasaidia wakulima kupata bidhaa hiyo bila usumbufu wa kutafuta namba kwa kuwa watakuwa ni watumiaji wa mwisho.

"Kuwe na ruzuku kama inavyofanyika kwenye sekta ndogo ya mafuta (dizeli na petroli), kwa watumiaji wake kutolazimishwa kuwa na namba ya usajili au vocha ili wahudumiwe kwa bidhaa zenye ruzuku," ilisema taarifa ya Mtutura.

Iliongeza: "Pia tunatoa rai kwa serikali kuweka mkazo wa kuimarisha mifumo ya matumizi ya mbolea mbadala (mbolea zisizo na kemikali) kutoka kwa wakulima wenyewe."

ACT-Wazalendo pia imeishauri serikali kulipa kwa haraka madai ya kampuni zinazosambaza mbolea ili kuepusha ucheleweshaji unaotokana na malimbikizo ya madeni yanayopunguza uwezo wa baadhi ya kampuni.

Alisema wakulima wanakabiliwa na changamoto za kiusajili na ucheleweshwaji wa namba za kuchukulia mbolea kutokana na kwamba unafanyika mjini na kuwafanya wakulima wasafiri umbali mrefu.

Alisema hali hiyo inayozorotesha shughuli za kiuzalishaji shambani hasa wakati huu ambao msimu wa kilimo umeanza.

Tayari msimu wa kilimo umeanza katika mikoa yenye uzalishaji mkubwa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Songwe, Tabora, Kigoma, Katavi, Lindi na Mtwara.




Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango, akisikiliza maelezo kutoka kwa Meneja wa Benki ya NBC Tawi la Kahama, Simon Ntwale (wa pili kushoto), kuhusu ushiriki wa benki hiyo, katika ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR, wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa kipande cha nne kutoka Tabora-Isaka, mkoani Shinyanga, eneo la Isaka mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PPRA yatetea 'Force Account'

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) imeeleza kuwa matumizi ya mfumo wa nguvu kazi ya ndani (Force Account) katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni njia inayofaa ikiwa itasimamiwa vyema.

Hayo yamebainishwa katika utafiti mdogo uliofanywa na mamlaka hiyo, ili kuangalia ufanisi wa utumiaji wa kikosi kazi katika miradi ya maendeleo ya ujenzi inayoendelea hapa nchini. Utafiti huo ulihusisha miradi 175 iliyofanywa kwa njia ya kikosi kazi.

Meneja Utafiti na Nyaraka wa PPRA, Nashon Masunya, akitoa ufafanuzi jana kuhusu suala hilo, alisema kuwa hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la matumizi ya njia hiyo katika miradi ya umma, hasa ujenzi wa shule, vituo vya afya, majengo ya ofisi za serikali na nyumba zinazomilikiwa na serikali.

Alisema ongezeko hilo limesababisha baadhi ya maeneo hoja nyingi kuibuliwa juu ya ukiukwaji wa maadili ya ununuzi na usimamizi wa mikataba na hivyo kupelekea matumizi makubwa ya fedha wakati wa utekelezaji wake.

Masunya alisema kuwa utafiti huo ulilenga kuangalia thamani ya fedha (Value for Money) na kuona kama njia hiyo ni sahihi kwa matumizi ya kutekeleza miradi ya maendeleo ili kuiwezesha mamlaka kutoa ushauri sahihi kwa serikali na wadau wengine wa maendeleo kuhusu matumizi yake.

"Tuliamua kufanya utafiti ili tuone kama njia hiyo ya Force Account ni salama kutumiwa na serikali kutokana na hoja nyingi zinazoibuliwa siyo tu na viongozi, bali hata wananchi," alisema.

Masunya alisema yapo maeneo ambayo yamefanikiwa katika utekelezaji wa miradi kwa kutumia njia hiyo licha ya baadhi ya maeneo mengine kushindwa kufanya vizuri.

Alifafanua kuwa PPRA ndiyo mamlaka yenye wajibu wa kusimamia ununuzi wa umma nchini, hivyo ina wajibu wa kuhakikisha thamani ya fedha na uwazi katika ununuzi unaonekana.

Akieleza zaidi kuhusu njia hiyo, ofisa huyo alisema sheria imeweka wazi kuwa yapo mazingira yanayoweza kulazimu taasisi kutumia njia hiyo.

Mazingira hayo ni kama taasisi inayotaka kutekeleza mradi inaona kazi hiyo siyo kubwa na maeneo ya mradi huo ni mbali kufikika.

Masunya alizikumbusha taasisi kuwa kigezo muhimu ni lazima zihakikishe kuwa wapo wataalamu ndani ya taasisi wanaoweza kusimamia na kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi.

Utafiti huo ulijumuisha miradi iliyofanywa katika sekta ya afya, maji na elimu kwa kutumia fedha za UVIKO-19. Utafiti huo uliangalia pia ukaguzi maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu Hesabu za Serikali (CAG) katika miradi ya sekta za elimu kwa mwaka 2020 na Ukaguzi Maalum uliofanywa na PPRA katika sekta ya afya mwaka 2020.

# India kuisaidia Tanzania uanzishaji vituo utafiti

**Na Romana Mallya**

SPIKA wa Bunge la India, Om Birla amelieleza Jukwaa la Biashara kati ya Tanzania na India (TIBF) kuwa nchi yao ipo tayari kuisaidia Tanzania kuanzisha vituo vya kujifunzia na utafiti katika masuala ya kilimo hasa eneo la kilimo hai.

Aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano ulioandaliwa na TIBF na kukutanisha ujumbe wa Bunge la India ambao umekuja Tanzania kwa ziara yenye lengo la kuimarisha uhusiano baina ya nchi hizo mbili.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam, Spika Birla alieleza furaha yake katika ziara hiyo nchini na kuzungumzia uhusiano wa kihistoria wa nchi hizo.

Alisema nchi yao ipo tayari kutoa msaada wa kiufundi wa aina yoyote katika nyanja zote.

Pia aliizungumzia Taasisi ya Teknolojia ya India (IIT) ambayo imekusudia kuanzisha tawi lake Tanzania kwa manufaa ya Watanzania ili kupata mafunzo.

Vilevile, alizungumzia uwekezaji unaofanywa katika sekta ya afya kwa kujengwa hospitali kubwa ya saratani Dar es Salaam.

Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan alizungumzia namna biashara kati ya nchi hizo mbili ilivyokua ndani ya miaka michache iliyopita kupitia ushirikiano uliopo wa kibiashara, kijamii na kiutamaduni.

Alisema India imeendelea kuwa mshirika wa pili mkubwa wa kibiashara na Tanzania na kwamba mipango kadhaa ya kuimarisha uhusiano huo wa kibiashara ipo mbioni ili kuzifanya nchi hizo kuwa bora na kufanya kazi zaidi mwaka huu.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mwenyekiti wa TIBF, Gagan Gupta alisema jukumu lao ni kukuza uhusiano wa kibiashara kati ya India na Tanzania.


HADITHI

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji analima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja wa wasichana warembo kijiji hapo ni mmoja waliopata shida hiyo. Hawana kwa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# Mtake Msitake - 15

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




Kulikuwa na mkanganyiko kwenye kuitikia, wengine walisema ipo na wengine haipo.

"Najua siasa safi ipo kwa viongozi wenu wa juu, lakini hapa nauliza kuna uongozi bora?"

"Hakuna baba." Akajibiwa kiasi cha kumfanya jamaa aliyekuwa akiuliza kutabasamu.

"Samahani sana kwa kuingilia sijui pati, hafla ya sherehe yenu, lakini sisi ni wageni wenu baadhi wametoka mkoani na wengine Dar es Salaam, tumekuja hapa kwa ajili ya kutetea maslahi ya taifa, kijiji chenu na wanakijiji kwa ujumla."

Kuna baadhi ya watu walianza kushangilia kwa nguvu bila kujua ni kitu gani kinataka kuongelewa.

"Tumekuja kuwaokoa wananchi wa kijiji hiki kutoka kwa watu madhalimu. Kuna watu mmewapa madaraka, lakini badala ya kuwasaidia na kuwalinda, wamewafanya kuwa watumwa."

Mpaka hapo tu, tayari wanakijiji ambao watoto wa mjini wanasema 'waliosomea Cuba' walishaanza kuelewa kuwa hao watu walio hapo ni wa aina gani na wamekuja kufanya nini. Hivyo wakaanza kushangilia kwa nguvu.

Wale wenzangu na mimi kwenye vichwa vigumu wakendelea kupatwa na mshangao wasielewe nini kinaendelea na kinachofanyika.

"Wananchi tumekuja hapa kuwarudishia tena kijiji kiwe mikononi mwenu na siyo mikononi mwa wakoloni weusi ambao wamewafanya watumwa. Tumepata habari kuwa hivi sasa mmekuwa watumwa ndani ya nchi yenu ya Tanzania na kijiji chenu hiki..."

Sasa hapo kila mmoja alijua sababu ya watu wale kuja pale. Ni kuwarudishia ardhi ambayo ilichukuliwa na mwekezaji zaidi ya asilimia 70 na wao kubaki na asilimia 30 tu.

Wakajikuta badala ya kuimba nyimbo zao za disco walizokuwa wakiimba awali, wakaanza kuimba 'ukombozi, umewadia, ukombozi umewadia." Waliimba kwa zaidi ya dakika tano.

"Ahsanteni sana wanakijiji, ahsanteni sana kwa kutuelewa mapema zaidi na kutuunga mkono. Sasa naomba tueleze kile kitu ambacho tumekusanywa na kuletewa Makao Makuu. Kama kuna kasoro kwa sababu nyinyi wenyewe mpo hapa mtaeleza."

**"Ahsanteni sana wanakijiji, ahsanteni sana kwa kutuelewa mapema zaidi na kutuunga mkono. Sasa naomba tueleze kile kitu ambacho tumekusanywa na kuletewa Makao Makuu. Kama kuna kasoro kwa sababu nyinyi wenyewe mpo hapa mtaeleza."**

Umati wa wanakijiji sasa ulizidi kumiminika zaidi. Hata wale ambao hawakuja kwenye sherehe hizo kwa sababu mbalimbali, walifika baada ya kwenda kuambiwa kuwa kuna watu ambao wamekuja kijijini hapo wanaoonekana kuwa wakombozi.

"Hapa kwenu kuna mtu mmoja alikuja miaka mitano iliyopita akitokea Arusha na kujitangaza kama ni mwekezaji, ndiyo siyo?"

Kelele za 'ndiyooo' zilizidi kusikika na kichoongezea sana hapo ni ngoma na vigelegele kutoka kwa kinamama.

"Sasa naomba utulivu, ili nieleze siri iliyofichika kwenye kijiji hiki.

"Ni kwamba mwekezaji alifika kwenye kijiji hiki cha Maweni na kuwatia mfukoni viongozi.

Akawapa rushwa na zawadi, kiasi cha kukubali kukaa naye kikao cha siri na kukubaliana kumuuzia asilimia 70 ya ardhi kwa madai ya kuwekeza.

Awali mliambiwa kuwa ardhi hiyo inatakiwa ya serikali kwa ajili ya kujenga zahanati, shule, kituo cha polisi na kliniki ya mama wajawazito.

Bila kujua hili wala lile wanakijiji mlikubali kwani waliona mtakuwa mmebarikiwa kuwa na kijiji cha kwanza kuwa na vitu vyote hivyo muhimu.

Mkatoa ardhi bila kusita, tena kukawa na sherehe kubwa kama hii ya leo, watu wakala na kunywa. Asilimia 30 ya ardhi iliyobaki mkagawana wananchi mkadanganywa haitamaliza ardhi yote, vingejengwa vitu hivyo ardhi ikibaki itarudishwa tena kwa wanakijiji waendelee na shughuli zao za kijamii kama kawaida. Hadi leo hii mwaka wa tano mmerudishiwa ardhi?"

"Hapanaaa."

"Zahanati, shule, kituo cha polisi na kliniki ya mama wajawazito zimejengwa?" Akauliza ofisa yule.

"Wapiii, waongo."

"Waongoeee"

"Ndiyo babaaa." Wanakijiji waliitikia na kuanza tena kushangilia kwa kupiga ngoma, sasa wakaanza kuimba

"Mosha Usonzo safari imemkumba. Mosha Usonzo safari imemkumba..."

"Naomba utulifu tafadhali ili tumalizie hili kwaza, kabla hatujaingia kwenye hatua nyingine.

Wanakijiji hao ambao walionekana kuchoshwa na umasikini mkubwa walioupata na wanaoendelea kuwa nao baada ya asilimia 70 ya ardhi yao kuchukuliwa, walinyamaza wamsikilize afisa huyo.

"Baada ya kuona hakuna dalili za ujenzi wanakijiji mlianza kuhoji na kuongea bila woga kuonyesha kutoridhishwa na hilo.

Viongozi waliokuwa mlungula na mwekezaji wakaa tena kikao, wakaona wawaongopee wanakijiji kwa kuwapa pesa kama wanakodisha. Mwekezaji sasa akaanza kuwatumia wanakijiji hao hao kama vibarua.

Ujanja uliotumika ni kwamba aliwapa kila mtu pesa kidogo, halafu ni kama alikuwa amewarudisha kila mmoja ardhi aliyokuwa akiimiliki ili waendelee kulima, lakini mazao alikuwa akiyachukua mwenyewe na kwenda kuyauza Dar es Salaam na mikoa akijipatia pesa nyingi na kuwalipa pesa ndogo. Ndivyo, sivyo?"

"Ndiyo mheshimiwaaa."

"Baada mwaka mmoja mwingine ndipo mlipoanza kuona athari ya walichofanya, kaanza kulalamika, lakini badala ya kujibu hoja yoyote aliyeonekana kupinga alishughulikiwa. Liliundwa kundi kama sungusungu, kazi ilikuwa ni kukamata, kuadhibu, kumtesa na kumuua yoyote yule anayeonekana kidomodomo wa kutaka kuwazindua watu."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MANGUNGU, ASHA BARAKA WAMWAGA SERA MSIMBAZI

**Na Saada Akida**

WAGOMBEA wa nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu wa Simba unaotarajiwa kufanyika Januari 29, mwaka huu jijini Dar es Salaam wameendelea kumwaga sera huku Murtaza Mangungu, mwenyekiti anayetetea nafasi yake, amesema anahitaji kuendeleza mazuri aliyoyafanya katika miaka minne iliyopita.

Katika nafasi hiyo, Mangungu anachuana na Moses Kaluwa.

Akizungumza jijini jana, Mangungu, alisema bado klabu iko katika mchakato wa kujenga uwanja wa kisasa ambao pia utakuwa na kumbi mbalimbali za mikutano.

"Wanachama naombeni ridhaa yenu ya kuongoza kwa mara nyingine, kuongoza nafasi hii ya uenyekiti wa klabu ya Simba ili kuendeleza mikakati ya maendeleo inayotarajiwa hasa kwa timu yetu kucheza hatua ya nusu au fainali ya Ligi ya Mabingwa.

Nikipata nafasi hii tena ndani ya Simba, niwahakikishie nitaendeleza pale tulipoishia. Hatuna muda wa kujadili kwa sababu yanaonekana kutokana na ushirikiano mkubwa wa baadhi ya klabu kubwa Afrika ikiwamo Al Ahly ya Misri na CSK Moscow katika mambo ya kiufundi," alisema Mangungu.

Aliongeza mipango ya bodi ya klabu hiyo ni kuifanya Simba kuwa bora zaidi na kujenga mifumo mizuri katika kuongeza mapato pamoja na kusimamia vyema soka la vijana.

"Kuhusu kukosa furaha hasa mechi na Yanga, msimu uliopita tulipoteza, sio kwa uzembe wa uongozi bali ilikuwa bahati mbaya, nitatumia nafasi inayofuata kufanya vizuri katika michuano yote tunayoshiriki bila kuangalia timu tunayokutana nayo," Mangungu alisema.

Naye Asha Baraka anayetetea nafasi ya Mjumbe Mwanamke katika Bodi ya Wakurugenzi alisema anawaomba wanachama wampe dhamana ya kuongoza tena katika nafasi hiyo ili aendelee kuwapa furaha.

Asha alisema anajivunia mafanikio ambayo Simba Queens imeyapata katika miaka minne aliyokabidhiwa timu ambapo ilifanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania kwa misimu mitatu mfululizo.

"Nimefanikiwa kwa kipindi chote kutwaa mataji mbalimbali kama Ligi Kuu, CECAFA ambayo mara ya kwanza tulikosa kwa kutofanya vizuri kutokana na ugeni wa mashindano lakini msimu uliopita niliongoza timu vyema na kufikia malengo yetu na kutetea ubingwa, lakini kwenda kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Asha.

Selemani Haroub, anayewania nafasi ya ujumbe kwa awamu nyingine anawaomba ridhaa wanachama ili kukamilisha kazi nzuri waliyoianza pamoja na viongozi waliokuwa madarakani.

"Mafanikio yaliyopatikana Simba ni kutokana na ushirikiano wenu wanachama, kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa, Simba kuwa katika nafasi ya 10 katika anga za kimataifa, kwa sasa malengo yetu ni kutwaa ubingwa Afrika, naomba ridhaa yenu ya kuwaongoza kwa mara nyingine ili kufikia malengo haya.

Naombeni nafasi nyingine ili kufanikisha ushindi na kufikia malengo, kutokana na kuwa ni sehemu ya watu waliofanikisha baadhi ya wachezaji wa Simba kutoka katika kituo changu akiwamo Beno Kakolanya na Oppa Clement," alisema Selemani.



Wachezaji wa mpira wa kikapu kutoka timu mbalimbali Dar es Salaam wakifanya mazoezi kwa ajili ya kulinda viwango vyao katika viwanja vya Jakaya Kikwete Youth Park, Dar es Salaam jijini jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Iramba yajipanga kuibua vipaji

**Na Jumbe Ismailly, IRAMBA**

WILAYA ya Iramba, mkoani Singida inatarajia kuanzisha mashindano ya soka yenye malengo ya kuwakutanisha vijana wa wilaya hiyo ili kuimarisha afya zao pamoja na kuendeleza vipaji vitakavyoibuliwa, imefahamika.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, ambaye ni mratibu wa mashindano hayo, Suleiman Mwenda, alisema maandalizi ya michuano hiyo yamekamilika na yataanza rasmi baada ya msimu wa kilimo kumalizika.

Mwendwa alisema mashindano hayo yatalenga pia kuimarisha sekta ya michezo katika wilaya hiyo na kujenga mahusiano imara kati ya mtu mmoja mmoja na wilaya yote.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Wazo Huru Media, Mathias Canal, alimpongeza mkuu huyo wa wilaya kwa ubunifu wa kuwakutanisha vijana katika kipindi hicho na anaamini itasaidia vijana waondokane na tabia ya kujihusisha na vitendo vibaya.

Canal alisema wameandaa mikakati mizuri kufanikisha vijana wanaendeleza vipaji vyao na mashindano hayo yatakuwa ni sehemu ya kuitangaza wilaya ya Iramba.

"Tutatumia mashindano haya kuinyanyua wilaya yetu na kuleta mapinduzi katika sekta ya uwekezaji wa michezo," Canal alisema.

## Taifa Jang'ombe kubakia Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Taifa Jang'ombe imesema itajipanga vyema ili kupata matokeo mazuri na hatimaye kuhakikisha inabakia katika Ligi Kuu Zanzibar, imeelezwa.

Taifa Jang'ombe ipo katika hali mbaya tangu kuanza kwa msimu huu baada ya kupata matokeo ya kusuasua katika mechi zake.

Kocha Mkuu wa Taifa Jang'ombe, Omar Khamis Matu, alisema wanahitaji kuongeza juhudi kwa kuwapa mbinu mbalimbali wachezaji wao ili kujinusuru janga la kushuka daraja wataanza kufanya mazoezi mara mbili kwa siku.

"Tumefungwa mchezo wetu wa kwanza kabisa wa mzunguko huu, lakini matumaini yetu makubwa timu itabadilika na wachezaji watafanya vizuri, ikizingatiwa nafasi tuliyoko lazima timu ipambane ili tushinde michezo inayofuata," Matu alisema.

Timu hiyo inayoburuza mkia ikiwa na pointi tisa kibindoni, itashuka tena dimbani keshokutwa kuwavaa Dulla Boys.

## Kundemba hasira zote kwa Kipanga

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LICHA ya kufungwa mabao 3-0 na KMKM katika mechi iliyopita, Kocha Mkuu wa Kundemba FC, Ali Vuai Shein, amesema kikosi chake kimejipanga kumaliza hasira zake kwa Kipanga ambao watakutana leo kwenye mchezo mwingine wa Ligi Kuu Zanzibar.

Matu aliliambia gazeti hili amesharekebisha makosa yaliyojitokeza katika mechi iliyopita na anaamini leo wataondoka na ushindi.

Shein alisema anafahamu mzunguko wa lala salama huwa mgumu na kuanza vibaya si kama kikosi chake kitaendelea kupotea.

Kocha huyo alisema timu yake ilifanya maboresho katika dirisha dogo la usajili kwa kuongeza nguvu kwenye safu ya ushambuliaji na ulinzi, hivyo anaamini matokeo mazuri yatapatikana.

"Hatupo katika nafasi nzuri katika msimamo wa ligi, ndio maana tulifanya usajili mdogo kulingana na mahitaji ya kikosi, ninamatumaini makubwa kikosi chetu kitaanza kupata ushindi kutokana na kiwango kizuri walichokionyesha katika mechi hii ya kwanza," Matu alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**CHELSEA KUMUUZA STERLING**
CHELSEA iko tayari kusikiliza ofa kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Raheem Sterling, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kuhamia Stamford Bridge msimu uliopita wa joto. ***(Football Insider)***

**RAPHINHA ANUKIA ARSENAL**
KLABU ya Arsenal imewasiliana na Barcelona ili kumnunua winga wa Timu ya Taifa ya Brazil, Raphinha, ambaye ana umri wa miaka 26. ***(90min)***

**BARCA KUMUUZA RAPHINHA**
BARCELONA imeweka bei ya euro milioni 100 kwa Raphinha, ambaye alihamia Nou Camp kutoka Leeds United Julai mwaka jana. ***(Sport)***

**BRIGHTON YAIGOMEA CHELSEA**
OFA ya Chelsea ya pauni milioni 55 kwa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ecuador, Moises Caicedo, mwenye umri wa miaka 21 imekataliwa na Brighton. ***(Mail)***

**NEWCASTEL KUSAJILI TISA**
KLABU ya Newcastle United ina orodha ya wachezaji tisa wa uhamisho ambayo ina mshambuliaji wa Everton na England chini ya umri wa miaka 21, Anthony Gordon na wachezaji watatu wa Chelsea. ***(Telegraph)***

**GUEDES KUTUA BENFICA**
MSHAMBULIAJI wa Wolves, Goncalo Guedes, mwenye umri wa miaka 26, yuko nchini kwao Ureno kabla ya kukamilisha uhamisho wa mkopo wa kujiunga na Benfica. ***(Matteo Moretto)***


**BELLINGHAM ATOA MSIMAMO**
KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya England mwenye umri wa miaka 19, Jude Bellingham, anatazamiwa kufanya mkutano wa uhamisho na Borussia Dortmund baada ya kuiambia Real Madrid anapendelea kuhamia Hispania. ***(Mirror)***

**LIVERPOOL VS BELLINGHAM**
KLABU ya Liverpool bado ina matumaini ya kumsajili Jude Bellingham. ***(Florian Plettenburg, Sky Germany)***

**SULEMANA ATAJWA EVERTON**
KLABU ya Everton inazungumza na Rennes kuhusu uwezekano wa kumnunua mchezaji wa kimataifa wa Ghana, Kamaldeen Sulemana, mwenye umri wa miaka 20. ***(Givemesport)***

**DAWSON KUTUA WEST**
KLABU ya Wolves imekubali mkataba wa pauni milioni 3.3 kumnunua beki wa West Ham, Craig Dawson, mwenye umri wa miaka 32. ***(Independent)***

**ARSENAL YAMFUATA ANTHONY**
ARSENAL inavutiwa na winga wa Bournemouth, Jaidon Anthony, mwenye umri wa miaka 23.***(Mail)***



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KIWANGO CHA CITY CHAMKERA GUARDIOLA

●●●Kocha huyo asema wanatakiwa kubadilika kwa sababu ushindani...

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola alikasirika na uchezaji wa nyumbani wa Manchester City na kusema haielewi timu yake katika hali ya sasa, licha ya ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Tottenham Hotspur.

City walizomewa nje ya uwanja wakiwa nyuma kwa mabao mawili katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi.

Hadi mapumziko, Spurs walikuwa wakiongoza kwa mabao 2-0 kabla ya City kurejea na magoli ya haraka ya kusawazisha.

Inakuwa mara ya pili kwa City kutokea nyuma mabao mawili na

fanya hivyo dhidi ya Crystal Palace hapo Agosti, mwaka jana.

Wakati ushindi huo umepunguza gepu na sasa wamepitwa pointi tano dhidi ya vinara Arsenal, ingawa walikuwa wamecheza mechi moja zaidi na Guardiola alisema hakufurahishwa na kile alichokishuhudia dhidi ya Tottenham.

Guardiola ameiambia Sky Sports; "Lazima tujiandae vyema zaidi. Siwezi kukataa jinsi tulivyo na furaha lakini tuko mbali na timu tuliyokuwa nayo, sio katika suala la uchezaji, tulicheza vizuri lakini kuna mambo mengine mengi kama vile ushindani."

Alipoulizwa ni nini kilikosekana

alisema: "Shauku, morali na hamu ya kutaka kushinda kutoka dakika ya kwanza. Mashabiki wetu walinyamaza kwa dakika 45. Walizomea kwa sababu tulikuwa tunapoteza lakini kipindi cha pili tulicheza vizuri, tulipata nafasi nyingi zaidi."

City wameshinda Ligi England katika misimu minne kati ya mitano iliyopita, huku viongozi wakishangazwa na Arsenal kuwinda taji la kwanza katika kipindi cha miaka 20.

Kikosi cha Guardiola bado kinapaswa kumenyana na Arsenal nyumbani na ugenini, lakini kocha huyo kutoka Katalunya amesisitiza timu yake haitawakamata washika-

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,067,6
MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
CHELSEA
1 | 1.83
X | 3.67
2 | 3.82
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# LINGARD: UNITED IKO NYUMA SANA

**MANCHESTER, England**

MCHEZAJI wa zamani wa Manchester United, Jesse Lingard, ametia chumvi kidonda baada ya kusema klabu hiyo ipo nyuma sana kwenye suala la miondombinu ukilinganisha na Manchester City na Tottenham Hotspur.

Lingard ambaye sasa anakipiga katika klabu ya Nottingham Forest amesema hayo baada ya miezi miwili nyuma aliyekuwa nyota wa klabu hiyo Cristiano Ronaldo kusema Manchester ipo nyuma sana kwenye suala ya miundombinu.

Mchezaji huyo alisema ukiangalia klabu kama Manchester City au Tottenham zenyewe zimejiimarisha sana nje ya uwanja katika suala la miundombinu, huku United ikiwa imeachwa mbali sana.

Lingard pia kwenye mahojiano yake alifunguka kuwa msimu uliomalizika alifikia hatua ya kutumia pombe ili aweze kuwa sawa kutokana na kipindi kigumu ambacho alikuwa anapitia ndani ya United kwenye msimu wa 2021/22.

Lingard amekua ndani ya United kwa miaka 22 kabla ya kuondoka kwa uhamisho huru ndani ya msimu huu na kutua Nottingham Forest.

Ameweka wazi alikuwa halali bila kunywa pombe kutokana na wakati mgumu aliokuwa anapitia ndani ya klabu hiyo na hiyo ni kutokana na kukosa nafasi na kufikia hatua hadi ya kutolewa kwa mkopo kwenda West Ham.

# Trossard ni mali ya Arsenal

**LONDON, England**


ALIYEKUWA winga wa Brighton Hove and Albion, Leandro Trossard amefanikiwa kujiunga na Arsenal, ambao kwa sasa ni vinara wa Ligi Kuu England.

Arsenal imefanikiwa kukamilisha dili la Trossard kutoka Brighton jioni ya juzi kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 27.

Dili la winga huyo limeenda haraka sana kutokana na hofu ambayo wamekua nayo Arsenal kwani wamepokonywa tonge mdomoni na Chelsea, hivyo walihitaji kukamilisha haraka iwezekavyo lisije likaingiliwa kama ambavyo walivyomkosa, Mykhaylo Mudryk.

Winga huyo wa kimataifa wa Ubelgiji anakwenda kuongeza nguvu ndani ya kikosi cha Arsenal ili kuhakikisha wanaendeleza ubora wao msimu huu na kuendelea kukimbiza ubingwa wa Ligi Kuu England ambao imeonekana klabu hiyo inauhitaji baada ya kuukosa kwa muda mrefu.

Taarifa kutoka klabu ya Brighton Hove and Albion imeeleza Trossard ameondoka ndani ya timu hiyo kutokana na kutokua na maelewano mazuri na kocha Roberto De Zerbi.



15,605/-


# MILIONI 22.7 ZATENGWA KILI MARATHON 2023 IKIZINDULIWA

**Na Mwandishi Wetu**




MBIO ndefu za kimataifa za Kilimanjaro International Premium Lager Marathon za mwaka huu zimezinduliwa rasmi Moshi, mkoani Kilimanjaro jana.

Mbio hizo zinazoandaliwa na Kampuni ya Kilimanjaro Marathon na kuratibiwa na Executive Solutions zitafanyika Februari 26, mwaka huu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkuu wa Mkoa wa Klilimanjaro, Nurdin Babu, aliyewakilishwa na Kaimu Mkuu wa mkoa huo, Abbas Kayande, alisema mbio za Kilimanjaro zimepiga hatua kubwa katika kukuza michezo hapa nchini na maadhimisho ya miaka 21 tangu kuanzishwa kwake ni taswira halisi ya jinsi waandaaji na wadhamini wa mashindano wako makini.

"Mwaka jana Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliagiza waandaaji wa Kilimanjaro Marathon ambayo pia yanatangaza utalii wa Tanzania kuanza kutumia jina ambalo litaonyesha mbio hizi ni za kimataifa na kweli mmeitikia wito huo na sasa mashindano haya yanajulikana kama Kilimanjaro International Marathon", alisema Babu.

Aliongeza mbali na kushiriki mbio hizi, washiriki pia wanapata fursa kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii kama kupanda Mlima Kilimanjaro, kutembelea hifadhi zetu za Taifa, mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Zanzibar.

Alisema serikali inajivunia kuhusishwa kwake na mbio hizo, moja ya mashindano makubwa ya kimataifa katika ukanda wa Afrika Mashariki, ambayo mwaka huu inatarajiwa kuwakutanisha washiriki zaidi ya 12,000 kutoka nchi zisizopungua 55.

"Mbio za Kilimanjaro Marathon zimechangia kwa kiasi kikubwa kukuza utalii wa michezo na hii imesaidia sana serikali katika azma yake ya kukuza sekta ya utalii nchini na sera ya Taifa ya utalii kwa ujumla.

"Nichukue nafasi hii kuwapongeza wadhamini wote wa mbio hizi wakiongozwa na mdhamini mkuu Kilimanjaro Premium Lager (42km), Tigo Half Marathon (21km) na Grand Malt 5km Fun Run kwa michango yao mikubwa, bila ya nyinyi pamoja na wadhamini wenza mashindano haya yasingekuwa na msisimko tunaouona sasa," alisema kiongozi huyo.

Alitoa pongezi zake kwa wadhamini wengine wa mashindano hayo ambao ni Simba Cement, Maji ya Kilimanjaro, TPC Sugar, Total Energies, Kampuni ya ulinzi ya GardaWorld Security, Keys Hotels, Kibo Palace Hotels na CMC Automobiles.

Neema Patrick, Meneja Mkuu wa Mauzo wa Kampuni ya Bia Tanzania Kanda ya Kaskazini, alisema wanajivunia kudhamini mbio hizo kwa mwaka wa 21 mfululizo.

Alisema mwaka huu wadhamini hao wamejipanga vyema kwa ajili ya mashindano ya 21 na kampuni imetenga Sh. milioni 22.7 kwa ajili ya zawadi mbalimbali.

Alitoa wito kwa washiriki kujiandikisha mapema ili kuepuka msongamano wa kupitia tovuti www.kilimanjaromarathon.com au TigoPesa kwa kupiga *150*01#. Aidha alitoa wito kwa washiriki wa mbio za kilomita 5 maarufu kama mbio za Burudani kujiandikisha mapema kwani idadi iliyopangwa ya washiriki ni ndogo tena.

Pia alitoa wito kwa wadhamini wenza katika mashindano hayo kujiandikisha kwa ajili ya mashindano ya ushirika ambapo watapata kukimbia kama vikundi na kwamba waandaaji watatoa muda maalum kwa ajili ya ushiriki wa vikundi ili kupata washindi katika kitengo hicho cha mashindano.

"Ushiriki wa makundi kupitia wadhamini wenza ni njia moja wapo ya kuleta wafanyakazi na wadhamini wote pamoja sambamba na kuboresha afya zetu," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo, alisema "Kama wadhamini wakuu wa kitengo cha mbio za kilomita 21 tunafurahia uzinduzi wa toleo la 2023 la mbio hizi ambazo zimepata heshima kubwa hapa nchini na duniani kote kwa sasa."

Zaidi ya hayo, alisema Tigo inafuraha kuendeleza mradi wake wa kupanda miti wakati wa msimu wa mbio hizo unaojulikana kama Tigo Green For Kili ikiwa ni jitihada na mchango wa kampuni hiyo katika kuhifadhi mazingira yanayozunguka Mlima Kilimanjaro.

# WACHEZAJI YANGA

INATOKA UK. 24

ni kurejea kwa Aucho ambaye alikuwa anasumbuliwa na majeraha ya kifundo cha mguu ameanza mazoezi mepesi jana (juzi), unapokuwa na wachezaji wote fiti, ni jambo jema kwa benchi la ufundi," kocha huyo alieleza.

Naye Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, ametamba timu yake imejipanga kuisimamisha Yanga ambao ndio vinara wa ligi hiyo ya juu nchini.

"Tumejipanga kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo, nimesikia sijui wamemleta Musonda (Kennedy), lakini sisi tutawachezesha msondo, wajipange kwa hilo, hatuna lingine tunaloweza kuwaambia," Bwire alisema.

Baada ya mechi hiyo, Yanga itabakia Dar es Salaam kuwasubiri Rhino Rangers katika mchezo wa hatua ya 32 bora ya mashindano ya Kombe la FA utakaochezwa kati ya Februari 27 na 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

# MGUNDA, MATOLA MALI YA SIMBA SC

INATOKA UK. 24

ochezwa kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini humo.

"Tumesafiri na wachezaji wote, hadi wapya waliosajiliwa hivi majuzi wamejumuishwa katika safari hiyo, kasoro wanne tu na wameachwa kwa sababu mbalimbali ikiwamo ya majeruhi ambao ni Mosses Phiri, Henock Inonga, Israel Mwenda na Peter Banda.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 21/01/23 | 18:00 | AFC Bournemouth vs Nottingham Forest | 2.60 | 3.20 | 2.65 |
| 02. 21/01/23 | 18:00 | Southampton FC vs Aston Villa | 2.80 | 3.30 | 2.42 |
| 03. 21/01/23 | 18:00 | Birmingham City vs Preston North End | 2.38 | 3.10 | 3.10 |
| 04. 21/01/23 | 18:00 | Blackpool vs Huddersfield Town | 2.27 | 3.15 | 3.20 |
| 05. 21/01/23 | 18:00 | Cardiff City vs Millwall FC | 2.95 | 3.05 | 2.48 |
| 06. 21/01/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Swansea City | 2.55 | 3.25 | 2.70 |
| 07. 21/01/23 | 18:00 | Wigan Athletic vs Luton Town | 2.75 | 3.15 | 2.55 |
| 08. 21/01/23 | 18:15 | Espanyol Barcelona vs Real Betis Seville | 2.80 | 3.15 | 2.55 |
| 09. 21/01/23 | 22:00 | SC Cambuur vs Sparta Rotterdam | 2.95 | 3.35 | 2.31 |
| 10. 21/01/23 | 23:00 | RKC Waalwijk vs Go Ahead Eagles | 2.36 | 3.45 | 2.80 |
| 11. 22/01/23 | 13:30 | Gaziantep FK vs Sivasspor | 2.50 | 3.30 | 2.75 |
| 12. 22/01/23 | 15:00 | Sunderland AFC vs Middlesbrough FC | 2.80 | 3.25 | 2.45 |
| 13. 22/01/23 | 16:30 | Feyenoord Rotterdam vs Ajax Amsterdam | 2.85 | 3.55 | 2.28 |
| 14. 22/01/23 | 17:00 | Leeds United vs Brentford FC | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 15. 22/01/23 | 17:00 | AC Monza vs Sassuolo Calcio | 2.26 | 3.30 | 3.10 |
| 16. 22/01/23 | 18:30 | Maritimo Madeira vs Estoril Praia | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 17. 22/01/23 | 19:30 | Borussia Monchengladbac vs Bayer Leverkusen | 2.70 | 3.80 | 2.31 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 21/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 4374 | Liverpool vs Chelsea | 1.83 | 3.67 | 3.82 |
| 15:30 | 5195 | Coventry vs Norwich City | 2.71 | 3.36 | 2.42 |
| 16:00 | 3799 | Rayo Vallecano vs Real Sociedad | 3.10 | 3.10 | 2.36 |
| 16:00 | 5906 | Genclerbirligi vs Boluspor | 2.96 | 3.21 | 2.22 |
| 16:00 | 5932 | Tanzania Prisons vs Ihefu FC | 2.13 | 2.70 | 3.30 |
| 17:00 | 1049 | Verona vs Lecce | 2.35 | 3.03 | 3.08 |
| 17:00 | 2269 | NK Osijek vs HNK Rijeka | 1.69 | 3.62 | 4.34 |
| 17:30 | 1720 | Eintracht Frankfurt vs Schalke 04 | 1.35 | 4.97 | 7.16 |
| 17:30 | 2067 | VfL Bochum vs Hertha BSC | 2.33 | 3.43 | 2.78 |
| 17:30 | 2728 | Union Berlin vs Hoffenheim | 2.16 | 3.31 | 3.16 |
| 17:30 | 3688 | VfL Wolfsburg vs SC Freiburg | 2.46 | 3.33 | 2.68 |
| 17:30 | 4737 | Stuttgart vs Mainz | 2.35 | 3.41 | 2.77 |
| 18:00 | 1306 | West Ham vs Everton | 1.74 | 3.56 | 4.45 |
| 18:00 | 1881 | QPR vs Swansea | 2.56 | 3.20 | 2.66 |
| 18:00 | 2069 | Arbroath vs Motherwell | 4.45 | 3.41 | 1.72 |
| 18:00 | 2075 | Stenhousemuir vs Livingston | 5.81 | 4.46 | 1.42 |
| 18:00 | 2195 | Leicester vs Brighton | 3.32 | 3.47 | 2.04 |
| 18:00 | 2491 | Southampton vs Aston Villa | 2.78 | 3.23 | 2.43 |
| 18:00 | 2680 | Stoke City vs Reading | 1.86 | 3.38 | 4.07 |
| 18:00 | 3887 | Bournemouth vs Nottingham | 2.68 | 3.07 | 2.63 |
| 18:00 | 4651 | Kilmarnock vs Dumbarton | 1.12 | 6.82 | 17.56 |
| 18:00 | 5079 | Birmingham vs Preston | 2.34 | 3.02 | 3.12 |
| 18:00 | 5276 | Hamilton vs Ross County | 3.99 | 3.32 | 1.82 |
| 18:15 | 3918 | Espanyol vs Betis | 2.69 | 3.14 | 2.64 |
| 18:30 | 4204 | Pacos Ferreira vs Sporting Braga | 6.39 | 4.39 | 1.45 |
| 19:00 | 1511 | Galatasaray vs Antalyaspor | 1.39 | 4.57 | 7.23 |
| 19:00 | 5674 | Altay vs Pendikspor | 3.52 | 3.21 | 1.98 |
| 19:30 | 4934 | Dinamo Zagreb vs HNK Gorica | 1.15 | 6.21 | 14.50 |
| 20:00 | 3841 | Salernitana vs Napoli | 8.87 | 5.52 | 1.27 |
| 20:00 | 4887 | FC Luzern vs FC Zurich | 2.12 | 3.51 | 3.13 |
| 20:15 | 1028 | The New Saints vs Bala Town | 1.26 | 5.36 | 8.45 |
| 20:30 | 2725 | Crystal Palace vs Newcastle | 4.07 | 3.42 | 1.85 |
| 20:30 | 3189 | FC Koln vs Werder Bremen | 2.18 | 3.66 | 2.87 |
| 20:30 | 5251 | Atletico Madrid vs Valladolid | 1.36 | 4.70 | 8.20 |
| 20:30 | 5862 | St Johnstone vs Rangers | 6.25 | 4.27 | 1.42 |
| 20:45 | 3821 | NEC Nijmegen vs Emmen | 1.93 | 3.27 | 3.91 |
| 21:00 | 1430 | Amazulu vs Marumo Gallants FC | 2.26 | 2.79 | 3.58 |
| 21:00 | 1541 | Kagera Sugar vs Coastal Union | 1.80 | 3.06 | 4.56 |
| 21:00 | 1942 | Santa Clara vs Benfica | 8.92 | 5.35 | 1.29 |
| 21:00 | 4602 | Kaizer Chiefs vs Mamelodi Sundowns | 4.17 | 3.32 | 1.86 |
| 21:30 | 4435 | Zamalek vs Al Ahly Cairo | 4.08 | 3.13 | 1.96 |
| 22:00 | 1462 | Cambuur vs Sparta Rotterdam | 2.98 | 3.17 | 2.33 |
| 22:00 | 2277 | Libya vs Ethiopia | 2.60 | 2.85 | 3.00 |
| 22:00 | 5157 | Mozambique vs Algeria | 7.20 | 3.85 | 1.49 |
| 22:00 | 5769 | PSV Eindhoven vs Vitesse Arnhem | 1.24 | 5.96 | 9.34 |
| 22:30 | 3870 | Grasshoppers vs BSC Young Boys | 4.25 | 3.98 | 1.70 |
| 22:45 | 5419 | Fiorentina vs Torino | 2.10 | 3.22 | 3.42 |
| 23:00 | 2569 | Sevilla FC vs Cadiz CF | 1.69 | 3.65 | 4.90 |
| 23:00 | 3682 | Waalwick vs GO Ahead Eagles | 2.37 | 3.36 | 2.77 |
| 23:30 | 4184 | Vitoria Guimaraes vs Porto | 6.97 | 4.68 | 1.39 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumamosi Januari 21, 2023

Nipashe



UKURASA 21

## Kiwango cha City chamkera Guardiola



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na mwigizaji maarufu wa filamu duniani kutoka Uingereza, Idris Elba (kulia), ambaye ni Balozi wa Hisani wa Umoja wa Mataifa wa IFAD baada ya kumaliza mkutano wa kuitangaza Tanzania katika sekta ya uwekezaji. Pia alifanya mazungumzo na Mwenyekiti Mwenza wa Klabu ya Manchester United, Avie Glazer (hayuko pichani). **PICHA: IKULU**

# WACHEZAJI YANGA KATIKA DOZI MPYA

## Nabi aongeza programu ya mazoezi ili kupata ushindi mnono na kujiweka...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwapa mapumziko ya siku moja, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, ametoa saa 48 kwa wachezaji wake kufanya mazoezi ya viungo ya gym kwa ajili ya kuimarisha pumzi kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting ya Pwani itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi, alisema uamuzi wa kufanya programu hiyo ya mazoezi unalenga kuongeza stamina ya wachezaji wake ambao wamerejea kutoka kwenye likizo fupi hivi karibuni.

Nabi alisema anataka kuwaona wachezaji wake wanakuwa na pumzi ya kutosha ya kukabiliana na ushindani kwa sababu kila mechi watakayocheza sasa ni ngumu na kila timu watakayokutana nayo inahitaji kuondoka na pointi.

"Nimewaandalia wachezaji wangu programu ya siku mbili ya gym, ilianza jana (juzi) na leo (jana), watamaliza, halafu watarejea tena uwanjani, nataka kuwaona wana pumzi ya kutosha kuwakabili wapinzani wakati wote, wawe wenye kustahamili kwa dakika 90 bila kuchoka," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema licha ya kupata ushindi, mechi iliyopita wachezaji wake walionekana kuchoka mapema huku wakiwa na pumzi ndogo hali ambayo haikuwa nzuri.

"Sio hawakuwa na pumzi kabisa, lakini harakati za kuboresha kikosi tu kwa kuwa tunahitaji kufanya vizuri tunatakiwa kutafuta mbinu mbalimbali za kumudu mapambano," alisema Nabi.

Aliongeza anahitaji kuona mchezaji anakuwa na uwezo wa kucheza kwa dakika 90 bila kuchoka, sio akikimbia kwa dakika chache anaonekana amechoka kama ilivyokuwa mechi iliyopita.

Alieleza kikosi chake pia kinajipanga kubadilisha mfumo wa uchezaji kutokana na mazingira watakayokutana nayo lakini kwa sasa wanaelekeza ngumu na akili kusaka matokeo mazuri dhidi ya Ruvu Shooting.

"Kwa sasa kikosi changu kimekamilika baada ya wachezaji wote waliokuwa mapumzikoni kumerejea nchini na kuungana na wenzao katika mazoezi, hii inaongeza hamasa na kuongeza ushindani wa kuwania namba kikosini," Nabi aliongeza.

Aliwataja nyota ambao wamerejea kikosini ni pamoja na Mghana, Benard Morrison, Yannick Bangala, Stephen Azizi Ki na Khalid Aucho.

"Habari njema ndani ya kikosi changu

INAENDELEA UK. 23

## Mgunda, Matola mali ya Simba SC

**Na Adam Fungamwango**

KUTOKANA na ujio wa Kocha Msaidizi mpya wa Simba, Ouanane Sellami, kutoka Tunisia, uongozi wa klabu hiyo umesema makocha wake wengine, Juma Mgunda na Selemani Matola, bado wataendelea kusalia katika kikosi hicho kilichotinga hatua ya makundi katika michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again', alisema uongozi umeleta kocha mwingine ili kuimarisha benchi la ufundi na wanaamini uamuzi huo utaongeza ufanisi.

Try Again alisema walihitaji kuona benchi la ufundi la Simba linakuwa na nguvu na uwezo wa kukamilisha majukumu yake vizuri na huo ndio 'ukubwa' na si vinginevyo.

"Licha ya kuboresha kikosi, sehemu nyingine ya muhimu ni benchi la ufundi, tumemleta Ouanane kama kocha msaizidi yakiwa ni mapendekezo ya kocha mkuu. Makocha wote waliokuwapo wataendelea kubakia, tulichofanya ni kuongeza nguvu," alisema Try Again.

Naye Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema huo ni mwendelezo wa maboresho ya benchi la ufundi kama ilivyokuwa kwa timu zilizoendelea za Afrika Kaskazini au barani Ulaya.

"Ni mwendelezo wa maboresho ya benchi la ufundi, ukienda kwa wenzetu walioendelea unakutana timu ina makocha mpaka 10 na watu wengine zaidi wa benchi la ufundi, kila kocha ana eneo lake la kufundisha na kulifanyia kazi. Kuna makocha wa viungo, mabeki, washambuliaji, fiziki, makipa, watu wa vyakula, saikolojia, yaani kila eneo lina mtu wake na huko ndiko tunakoelekea, Simba hatuwezi kuwa na kocha mmoja tu kama Mungu," alisema Ahmed.

Aliongeza kikosi chao kitaendelea kuwa na wataalamu wengi kwa ajili ya kujiongezea maarifa kwa sababu malengo yao makubwa ni kufanya vizuri katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Ili ufike huko lazima ukusanye watu (makocha) wengi waje kukufanyia kazi," alisema Ahmed.

Aliongeza kikosi chao kiliondoka Dar es Salaam jana jioni na kuelekea Dodoma kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara Dodoma Jiji FC itakay-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >